# RIPOTI YA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

## SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Uchumi ni miongoni mwa Kamati nane za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu Kanuni ya 107, Jadueli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020. Kamati hiyo imepangiwa kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
ii. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadiri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;
iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na ya Wananchi ya Wizara husika;
iv. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
v. Kuchambuwa mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
vii. Kuchambuwa ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika;

Katika kutekeleza majukumu yaliyopo hapo juu, Kamati ya Uchumi inasimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara tatu zifuatazo:

- Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji
- Afisi ya Rais, Fedha na Mipango
- Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

## 1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi ina Wajumbe wanane wafuatao:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Juma Makungu Juma - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamza Hassan Juma - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
6. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman - Mjumbe
7. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf - Mjumbe
8. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

Aidha, Kamati ina makatibu wawili ambao ni:

1. Ndg. Nouman Thabit Nouman - Katibu
2. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Katika utekelezaji wa kazi zake chini ya Jadueli la Kwanza la Kanuni ya 107 ya Baraza la Wawakilishi toleo la 2020, Kamati ilifanya kazi kwa utaratibu wa kupokea taarifa tofauti za kila robo mwaka (quarterly reports) za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara,kupokea taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamatipamoja na kukagua baadhi ya maeneo na

miradi mbali mbali inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kutoa ushauri wa kutatua changamoto hizo.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ilifanya kazi zake kwa mizunguko miwili (2) kwa muda wa wiki nne (4), Unguja na Pemba.

1. Mzunguko wa kwanza ulianzia tarehe 18 Januari, 2021 hadi tarehe 29 Januari, 2021 Unguja.
2. Mzunguko wa pili ulianzia tarehe 22 Machi, 2021 hadi tarehe 24 Machi, 2021 Pemba na tarehe 25 Machi, 2021 hadi tarehe 01 Aprili, 2021 Unguja.

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ilifanya kazi kwa mizunguko mitatu kwa Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

1. Mzunguko wa kwanza ulianzia tarehe 09 Agosti hadi tarehe 13 Agosti 2021 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 16 Agosti hadi tarehe 20 Agosti 2021 kwa upande wa Unguja.
2. Mzunguko wa pili ulianzia tarehe 15 Novemba 2021 hadi tarehe 19 Novemba 2021 Tanzania Bara na kuanzia tarehe 22 Novemba hadi tarehe 26 Novemba 2021 kwa upande wa Unguja.
3. Mzunguko wa tatu ulianza tarehe 17 Januari 2022 hadi tarehe 21 Januari 2022 kwa upande wa Pemba na kwa upande wa Unguja Kamati ilianza tarehe 24 Januari 2022 hadi tarehe 28 Januari 2022.

## SEHEMU YA PILI

## AFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO

## 2. UTANGULIZI

Afisi ya Rais, Fedha na Mipango imeundwa na mafungu makuu matatu ambayo ni Afisi ya Rais Fedha na Mipango (F01), Mfuko Mkuu wa Serikali (F02) na Tume ya Mipango (F03). Mafungu hayo yameundwa na Idara kumi (10), Taasisi nane (08) zinazojitegemea na Taasisi nne (04) za Muungano zinazofanya kazi hapa Zanzibar.

### 2.1 UKUSANYAJI MAPATO KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA (JULAI- DISEMBA 2021)

Kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021, jumla ya shilingi 440.59 bilioni zilikusanywa sawa na asilimia 72 ya makadirio ya kukusanya shiingi bilioni 609.76 kwa kipindi hicho. Makusanyo hayo yanajumuisha mapato ya kodi ya jumla ya shilingi 170.11 bilioni zilizokusanywa na ZRB, sawa na asilimia 64 ya malengo ya 263.79 bilioni. Aidha, jumla ya shilingi 164.59 bilioni zimekusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) sawa na asilimia 82 ya makadirio ya shilingi 201.12 bilioni. Kadhalika, mapato yasiyokua ya kodi ya shilingi 28.46 bilioni sawa na asilimia 42 ya lengo la shilingi 67.40 bilioni ambapo mapato kutoka kwa washirika wa Maendeleo yaliyokusanywa ni jumla ya shilingi 77.43 bilioni sawa na asilimi 100 ya makadirio.

### 2.2 MATUMIZI JULAI HADI DISEMBA 2021

Afisi ya Rais, Fedha na Mipango ilipanga kutumia jumla ya shilingi 172.17 bilioni kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021. Hadi kufikia Disemba 2021, Kamati iliarifiwa kuwa matumizi halisi yamefikia jumla ya shilingi 116.13 bilioni sawa na asilimia 67.
Matumizi hayo yanajumuisha TZS 22.58 bilioni ni matumizi ya OR - Fedha na Mipango, fungu F01 ambayo ni sawa na asilimia 35 za makadirio ya TZS 64.77 bilioni; TZS 86.73 bilioni ni matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali, fungu F02 ambayo ni sawa na asilimia

89 ya makadirio ya TZS 97.09; na TZS 5.02 bilioni ni matumizi ya Tume ya Mipango, fungu F03 ambayo ni sawa na asilimia 49 ya makadrio ya TZS 10.31 bilioni. Matumizi OR - Fedha na Mipango (F01).

## CHANGAMOTO ZA WIZARA KWA UJUMLA

1. Taasisi zinazosimamiwa na Wizara hazipati taarifa za kazi kwa wakati jambo ambalo hupelekea kutokuwa na ufanisi wa kazi.
2. Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma inakabiliwa na:
    - Uhaba wa vyombo vya usafiri unaopelekea kushindwa kufuatilia shughuli za kikazi kwa ufanisi.
    - Maslahi madogo kwa watendaji wa Mamlaka hii ambayo inahusika moja kwa moja na manunuzi ya fedha nyingi.
3. Baadhi ya Miradi inayosimamiwa na Wizara inatoa fursa mbalimbali za kuwainua wananchi kiuchumi lakini wananchi hao hawana taarifa kamili juu ya fursa hizo. Kamati imearifiwa juu ya fursa zinazotokana na mradi wa MKURABITA ambazo bado hazijatumiwa kutokana na kukosa taarifa hizo.
4. Uhaba wa wataalamu katika fani za TEHAMA jambo ambalo huigharimu Serikali kutafuta wataalamu wan je ya ofisi ili kusaidia utekelezaji wa majukumu yake.
5. Uchakavu wa jengo na uhaba wa ofisi unapelekea kupunguza ufanisi wa kazi.

## 2.3 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), umeanzishwa chini ya sheria nambari 2 ya mwaka 1998 ambayo ilifanyiwa mapitio makubwa na kuundwa upya na sheria nambari 2 ya mwaka 2005 na kufanyiwa tena marekebisho kwa sheria nambari 10 ya mwaka 2016. Mfuko unaendesha uwekezaji mbali mbali kwa lengo la kupata mapato ya uwekezaji ili kuweza kumudu uendeshaji wake.

Kwa upande wa Uwekezaji, mfuko umewekeza jumla ya shilingi 617,682,716,263.83 kwenye maeneo mbali mbali kama ifuatavyo:

| NA. | AINA YA UWEKEZAJI | KIWANGO | UHALISIA (%) |
|---|---|---|---|
| 1 | Uwekezaji katika mabenki | 78,070,613,915.77 | 13% |
| 2 | Hati fungani za Makampuni | 16,500,243,915.43 | 3% |
| 3 | Dhamana za Serikali | 47,358,022,816.58 | 8% |
| 4 | Hati fungani za Serikali | 234,458,429,677.40 | 38% |
| 5 | Mikopo | 8,973,153,392.68 | 1.5% |
| 6 | Majengo | 160,486,412,910.34 | 26% |
| 7 | Ruzuku za Ardhi | 35,970,700,000.00 | 6% |
| 8 | Hisa | 35,865,139,635.63 | 6% |
|  | JUMLA | 617,682,716,263.83 | 100% |

Aidha, mfuko umewekeza kwenye Majengo ambayo yapo Unguja na Pemba.

a) Mbweni Mpya
b) Mbweni Kongwe
c) Mwanakwerekwe Shopping complex
d) Kiwanja cha kufurahishia watoto (kariakoo na tibirinzi )
e) Michenzani Mall
f) Thabit Kombo Mall
g) Chawl (Jumba la Treni)
h) ZSSF Conference centre (Pemba)

i) Mkoani Hotel Pemba

**j)** ZSSF Office-Tinirinzi Pemba

## CHANGAMOTO

1. Mfuko umekumbwa na janga kubwa lililotokana na mripuko wa UVIKO-19 duniani ambalo limeathiri ukusanyaji wa michango ya wanachama kutoka katika sekta binafsi hususan sekta ya utalii kwa takriban asilimia 25.

2. Mfuko ulitarajia kulipa pencheni kwa wastaafu 10,854 lakini ulilipa wastaafu10.93 sawa na100.70 % ya wastaafu waliotarajiwa kulipwa, pia jumla ya shilingi 7,334,736,925 bilioni zilitegemea kulipwa kama pencheni lakini zililipwa jumla ya shilingi 9,105,816,464 bilioni sawa na 124 % ya makisio ya pencheni. Hali hii imesababishwa na uwepo wa taarifa tofauti za tarehe za kustaafu kwa wafanyakazi mbali mbali hivyo kupelekea tofauti ya makisio ya malipo na uhalisia wakati wa kustaafu.

3. Kutokana na baadhi ya waajiri kupunguza wafanyakazi wao raia wa kigeni, Mfuko ulitarajia kulipa marejesho kwa wanachama187lakini waliolipwa ni 121 sawa na 64% jumla ya shilingi 1,497,722,905 bilioni zilitarajiwa kutumika kama marejesho lakini zilitumika shilingi 1,668,378,160 bilioni ambazo sawa na 111% .

4. Baadhi ya waajiri hasa wa taasisi binafsi na mahoteli kutofuata sheria nambari 2 ya mwaka 1998 ambayo ilifanyiwa mapitio makubwa na kuundwa upya na sheria nambari 2 ya mwaka 2005 na kufanyiwa tena marekebisho kwa sheria nambari 10 ya mwaka 2016, kwa kutowachangia waajiriwa wao.

5. Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya jamii kutoingizwa kwenye kanuni za Utalii (Zanzibar Tourism Act) hasa kanuni ya 4 ya Kanuni za Utalii ya Mwaka 2015 ambayo inaitambua ZRB na TRA tu, hivyo kupelekea wafanya biashara ya utalii

kuona ni hiari kuwasajili na kuwachangia waajiri wao, jambo ambalo limepelekea wafanyakazi wengi wanaofanya kazi kwenye taasisi zinazojishughulisha na biashara ya utalii kukosa hifadhi yao ya jamii ya Maisha ya baadae.

6. Baadhi ya Miradi ya mfuko wa Hifadhi ya jamii inapata changamoto kwenye malipo ya kodi ya uwekezaji wa majengo kutoka kwa wafanya biashara au wanunuzi wa nyumba zilizoekezwa, hali inayopelekea kuilazimu ZSSF kutumia nguvu kwenye ukusanyaji wa mapato au kodi za miradi yake.

7. Mfuko wa Hifadhi ya jamii unaendelea kutoa mikopo kwa Serikali na taasisi kubwa lakini urejeshwaji wa mikopo hiyo umekua wa kusuasuana hivyo kupelekea uwezo wa mfuko katika uwekezaji kupungua.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Ili kuwa na Miradi inayoleta tija kwa wanachama wa mfuko na wananchi kwa ujumla, Kamati inashauri Mfuko ufanye utafiti wa kina juu ya ulipaji wa miradi hiyo kabla ya kuanza kutekelezwa.
2. Kamati inashauri Mfuko kutafuta maeneo ya kimkakati kwa ajili ya kuwekeza ambayo yatakuwa na uhakika wa kupata marejesho kwa muda mfupi na kuendeleza ustawi wa mfuko.
3. Kumejitokeza miradi ambayo ilianzishwa kupitia mfuko wa ZSSF na baadae kuishia njiani. Hivyo, Kamati inashauri miradi iliyohakikiwa na kuanzishwa iendelezwe kwa maslahi ya Taifa.

## 2.4 SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Shirika la Bima la Zanzibar ni shirika la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lililoanzishwa mwaka 1969 na linaendeshwa kwamujibuwa sheria ya Mitaji ya Umma Namba 4 ya mwaka 2002 na sheria ya Bima Namba 10 ya mwaka 2009.Ni shirika lililosajiliwa na Kamishna wa Bima Tanzania kutoa huduma za bima katika mfumo wa bima ulioanzishwa mwaka 1998 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati

iliarifiwa kuwa Shirika lina jumla ya watumishi 110 ambao wanajumuisha watumishi wakudumu 57 na 53 wa mkataba.

Majukumu makuu ya ya Shirika ni kama ifuatavyo:

- Kutoa huduma ya kinga za Bima za aina mbalimbali kwa jamii
- Kuwekeza katika miradi mbalimbali ya maendeleo

Kwa kipindi cha Julai/Disemba 2020 shirika lilijipangia kukusanya jumla ya shilingi 14.5 bilioni kutoka katika vyanzo vyakevya mapato na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 10.3 bilioni sawa na asilimia 71 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Shirika liliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi TZS 5.1 bilioni kwa kazi za kawaida kwa kipindi cha Julai/Disemba 2020 ambapo Kamati iliarifiwa kuwa ni jumla ya shilingi TZS 3.6 bilioni ndizo zilizotumika katika kipindi hicho sawa na asilimi 71 ya makadirio.

Aidha, Shirika limefanya matumizi ya jumla ya shilingi TZS 420.36 milioni kwa kazi za maendeleo ili kukidhi mahitaji ya maendeleo kwa kipindi cha Julai/Disemba 2020 na kulipa gawio la shilingi TZS 400 milioni kutokana na faida iliyopatikana. Sambamba na hayo, Shirika limefanikiwa kuchangia jumla ya shilingi450 milioni kwa ajili ya uanzishwaji wa kiwanda cha mwani nchini kati ya shilingi bilioni 1 ambazo lilipangiwa kuchangia.

**Kwa upande wa Kanda ya Pwani**, Afisi ya Bima ilianzishwa mwaka 2000 ikiwa na watendaji watano (5) katika eneo la Kitumbini na baadae kuhamia mtaa wa Mosque mwaka 2004 na hatimae kuhamia kwenye eneo la Lumumba ikiwa na jumla ya watendaji (24). Afisi inashirikiana na Mawakala 33 pamoja na madalali (4).

Kwa mwaka 2021, Afisi ya Kanda ya Pwani ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 14,154,936,932 bilioni ambapo hadi kufikia Oktoba 2021 jumla ya shilingi 8,058,520,725.02 bilioni sawa na asilimia 68.32 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Afisi ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,096,061,221.38 bilioni ambapo ilitumia jumla ya shilingi 5,898,885,698.38 bilioni sawa na asilimia 72.86 ya matumizi.

Kwa ujumla, Afisi imejipangia kuongeza idadi ya mawakala na madalali pamoja na kuongeza mashirikiano na mabenki katika kufanya biashara ya bima (bankassuarance).

**Kwa upande wa Kanda ya Ziwa,** Shirika limeanza kutoa huduma katika mikoa minane (8) kuanzia mwaka 2002. Mikoa hiyo ni Mwanza, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Kagera, Geita, Mara na Simiyu. Afisi ina jumla ya watandaji sita (6) na mawakala ishirini na tano (25) walioenea katika sehemu mbali mbali za kanda, ikiwa na jumla ya wateja 8572.

Kwa mwaka 2021, Afisi ya Kanda ya ziwa ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 545,701,200milioni ambapo hadi kufikia Oktoba 2021, jumla ya shilingi 370,507,069.66 milioni sawa na asilimia 67.89 ya makadirio.

Kwa upande wa matumizi, Afisi ya Kanda ya ziwa ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 8,096,061,221.38 bilioni ambapo kiuhalisia ilitumia jumla ya shilingi 5,898,885,698.38 bilioni sawa na asilimia 72.86 ya makadirio.

Kwa kipindi cha Januari – Disemba 2021, Afisi ya Kanda imelipa jumla ya shilingi 178,300,649.61 milioni kwa ujira wa mawakala. Aidha, ofisi imelipa jumla ya shilingi 210,722,217 milioni sawa na asilimia 45 ya makadirio ya kiasi cha shilingi 472,500,000 milioni.

## CHANGAMOTO

1. Baadhi ya mawakala wa huduma za bima hufanya kazi na kampuni zaidi ya moja jambo ambalo hupelekea kutoa huduma kwa upendeleo wa kampuni Fulani.
2. Mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO - 19 umesababisha kusimama kwa shughuli nyingi za kiuchumi na hivyo kupelekea pia kushuka kwa mauzo ya bima kutoka kwa wateja.

3. Madeni makubwa ambayo shirika linazidai taasisi za umma na binafsi ni tatizo kwa ukuaji wake.
4. Kuchelewa kulipiwa bima kwa baadhi ya vyombo vya taasisi za Serikali likiwemo Shirika la meli.
5. Ukosefu wa majengo ya ofisi Tanzania bara na Pemba umepelekea shirika kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kukodi majengo. Kiasi cha shilingi TZS 600 milioni hulipiwa majengo ya ofisi kwa mwaka.
6. Baadhi ya Kampuni za Bima hazifuati taratibu za uandikishaji bima, hasa katika matumizi ya viwango elekezi (rate) inayotolewa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA).
7. Kanda inakabiliwa na changamoto pale inapotokea kufanya kazi na wafanyakazi wasio waadilifu katika taasisi mbali mbali kama polisi, Mahakama na Hospitali kwa kutoa nyaraka za kughushi.
8. Baadhi ya taasisi za Muungano bado hazijalikubali Shirika la Bima la Zanzibar kama shirika la Serikali.
9. Katika kanda ya ziwa, Shirika linakabiliwa na ukosefu wa mtaalamu wa kufanya uchunguzi (investigation officer) na hulazimika kutumia wataalamu wa nje ya ofisi kwa njia ya mikataba.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuifanyia marekebisho sheria ya "Motor Vehicle Third Party Risk Decree Cap 136" ambayo ilitungwa mwaka 1953 na kubainika kuwa viwango vya tozo zake vimepitwa na wakati na vinalikosesha Shirika Mapato.
2. Ili Shirika litengeneze faida kutokana na biashara ya bima, Kamati inazitaka taasisi za umma na za binafsi kulipa madeni yake yote. Katika kufanikisha azma hii, Shirika liziandikie barua za ukumbusho taasisi zenye madeni.
3. Kamati inaiomba Serikali kutoa mwongozo kwa mashirika na Taasisi za Serikali za Tanzania Bara kwa kulitambulisha Shirika la Bima la Zanzibar kuwa ni taasisi ya Serikali.

4. Ni vyema Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) kuchukua hatua kali kwa Makampuni ambayo hayafuati miongozo ya Serikali.
5. Kituo cha Shirika la Bima Kahama kinapaswa kuwa na watendaji alau watatu ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa kwa ufanisi zaidi badala ya watendaji wawili ambao Kamati iliripotiwa.
6. Kamati inalishauri Shirika la Bima la Zanzibar kutoa huduma ya bima ya bure kwa gari maalum ikiwa ni sehemu ya matangazo kwa Tanzania Bara kwa nia ya kumudu ushindani wa biashara uliopo.
7. Ni wajibu wa Shirika la Bima la Zanzibar kuendelea kutoa elimu ya bima kwa jamii kwani Kamati imebaini kuwa wananchi walio wengi hawana uelewa wa masuala ya bima.
8. Kwa maslahi mapana ya Shirika na Serikali kwa ujumla, Kamati inazitaka taasisi za Serikali kukata bima zao zote za vyombo, majengo na miradi wanayoisimamia kwenye Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC).
9. Kamati inaishauri Serikali kununua majengo kwa pamoja kwa ajili ya taasisi zenye matawi Tanzania Bara ili kuziepusha taasisi hizo na mzigo mzito wa kadi ambao unapunguza uwezo wa taasisi hizo.

## 2.5 MAMLAKA YA USIMAMIZI WA BIMA TANZANIA (TIRA)

Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) imeanzishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5(1) cha sheria ya Bima Namba 10 ya mwaka 2009 ikiwa na majukumu ya msingi yafuatayo:

i. Kusajili makampuni ya Bima, Mawakala, Madalali, Wakadiriaji hasara wa mali na ajali.
ii. Kukagua na Kusimamia utendaji wa shughuli za bima.
iii. Kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusiana na huduma za Bima na
iv. Kutoa elimu ya Bima kwa umma.

Mamlaka inaongozwa na Kamishna aliye na Ofisi Tanzania Bara (Dodoma) na Naibu Kamishna aliye na Ofisi Zanzibar. Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake, Mamlaka ina Ofisi katika Kanda nne; Kanda ya Kaskazini inayohudumia mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga. Kanda ya Ziwa inayohudumia mikoa yote ya Kanda ya ziwa na Kigoma, Kanda ya Kati inayohudumia mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida na Morogoro. Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayohudumia mikoa ya Mbeya, Iringa, Katavi, Songe, Rukwa na Njombe.Kanda ya Mashariki inayohudumia mikoa ya Dar-es-salaam,Pwani, Lindi na Mtwara. Ofisi ya Zanzibar inayohudumia mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Katika kipindi cha mwaka 2020, sekta ndogo ya bima ilikua kwa asilimia1.6 kwa mauzo yenye thamani ya bilioni 827.86. Hata hivyo, kiwango cha bima za kawaida kimepungua kutoka shilingi 694.9 bilioni mwaka 2019 hadi shilingi 690 bilioni mwaka 2020 sawa na asilimia 0.7 ya upungufu. Kamati iliarifiwa kuwa hali hii imetokana na athari za
UVIKO -19.

Kwa upande mwengine, watumiaji wa huduma za bima nchini wameongezeka kwa asilimia 5.14 mwaka 2019 kutoka watumiaji 5,709,878 hadi watumiaji 6,003,239 mwaka 2020. Idadi hii ni ndogo kulingana na malengo yaliyopangwa.

Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Mamlaka inaendelea kutekeleza Mkakati wa miaka mitano wa Uendelezaji soko la Bima (TIRA –Corporate Strategic Plan 2020 – 2025). Aidha, kwa kushirikiana na wadau mbali mbali, Mamlaka imeandaa mkakati wa upelekaji wa elimu kwa umma wa miaka mine (National Insurance Education Srtategy – 2021- 2025) ambao utapelekea asilimia 78 ya wananchi wanapata uelewa wa masuala ya bima. Hadi kufikia 2029/30, watumiaji wa huduma za bima nchini wataongezeka kutoka asilimia 15 ya sasa hadi kufikia asilimia 50.

## CHANGAMOTO

1. Upungufu wa kiwango cha bima za kawaida uliosababishwa na janga la UVIKO-19 linaloikabili Dunia kwa sasa.
2. Kutokuwa na kampuni ya bima inayotoa huduma ya bima ya Kimataifa ambapo baadhi ya wateja wanahitaji huduma hiyo.
3. Sheria ya ya Usajili wa Makampuni inahitaji kufanyiwa marekebisho.
4. Sera ya Bima ya Taifa imeandaliwa kwa muda mrefu sasa lakini bado haijaanza kutumika.
5. Kutokuwa na Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ambayo ndio chombo kikuu cha maamuzi ya taasisi ambacho kimekosekana tangu mwaka 2019.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa Sera ya Bima ya Taifa (National Insurance Policy) ili kuwa na dira ya utekelezaji wa majukumu yake.
2. Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli zake, Kamati inashauri Serikali iunde Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ambayo ndio chombo kikuu cha maamuzi ya taasisi ambacho kimekosekana tangu mwaka 2019.
3. Kamati inashauri kutolewa kwa taaluma ya stickerless kwa jeshi la Polisi nchini ili kuepusha migogoro isiyo ya lazima baina yao na wateja wa bima barabarani.
4. Kamati inaiomba Serikali kupitia (TIRA) kuipitia upya Investment ratio ya mashirika ya Bima na kupunguza kiwango hicho ili kuyapa nafuu mashirika hayo na kuyafanya yapate maendeleo ya haraka.
5. Kwa mujibu wa mwongozo wa Sheria ya Usajili wa Makampuni, umejitokeza ugumu wa biashara ya bima nchini na hivyo, Serikali inahitaji kulishughulikia suala hilo ili kulitafutia ufumbuzi wake.

## 2.6 BENKI KUU YA TANZANIA (BOT)

Benki Kuu ya Tanzania ilianzishwa mwaka 1966 kwa sheria ya Bunge yam waka 1965 ili kutekeleza majukumu ya msingi ya Benki Kuu kama zilivo benki kuu nyengine duniani. Kwa sasa, Benki Kuu ya Tanzania inaendeshwa chini ya sheria ya Benki Kuu ya Tanzania,

Namba 4 ya mwaka 2006 ambapo kifungu cha 5 hadi cha 7vinaelezea majukumu yake. Kwa ajili ya utekelezaji bora wa majukumu hayo, sheria nyengine pia hutumiwa na Benki Kuu ya Tanzania kama Sheria ya Fedha za Kigeni Namaba 1 ya mwaka 1992, Sheria ya mifumo ya Taifa ya Malipo Namba 4 ya mwaka 2015, Sheria ya Usimamizi wa mabenki na Taasisi za Fedha Namba 5 ya mwaka 2006 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Namba 10 ya mwaka 2018.

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Benki Kuu inaongozwa na Gavanaakisaidiwa na Manaibu Gavanawatatu ambao wote wameteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wa Zanzibar, shughuli za Benki Kuu zilianza rasmi tarehe 28 Machi 1988 na kuchukua nafasi ya Ofisi ndogo iliyokua ikitoa huduma za kifedha kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tangu mwaka 1967. Mnamo mwaka 2002, akaunti za Serikali (SMZ) zilihamishiwa Benki Kuu kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) ambayo ilikua ikifanya kazi kama Benki kwa Serikali (Banker to the Government).

Mkurugenzi ndiye Mtendaji Mkuu wa Benki Kuu – Zanzibar ambaye anasaidiwa na Mameneja watatu wanaoshughulikia uchumi, uendeshaji na Utawala na Fedha ambao pia husimamia jumla ya watendaji 64. Kimsingi, majukumu ya Benki Kuu kwa upande wa Zanzibar ni:

- Kutoa huduma za kibenki kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zilizopo Zanzibar.
- Kutoa ushauri wa Kiuchumi kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar
- Kutoa huduma za kibenki kwa benki za biashara zilizopo Zanzibar
- Kutoa na kusambaza fedha
- Kufuatilia mwenendo wa Uchumi wa Zanzibar
- Kufanya tafiti za Kiuchumi
- Kushiriki katika vikao vya Serikali
- Kusaidia katika utoaji wa huduma za kijamii (corporate social responsibility)

## CHANGAMOTO

1. Uelewa mdogo wa wananchi juu ya kazi na majukumu ya Benki Kuu ya Tanzania
2. Wananchi walio wengi kutoelewa juu ya fursa za uwekezaji katika masoko ya fedha.
3. Wananchi kutokua na uelewa wakutosha wa namna ya kizitambua noti halali na kujiepusha na upokeaji wa noti bandia.
4. Bado wananchi walio wengi wanapendelea kufanya malipo kwa fedha taslimu
5. Wadau wa sekta ya fedha nchini kuwa wazito kwenye utoaji wa taarifa zinazohitajika katika tafiti zinazofanywa na Benki Kuu.
6. Kushindwa kupata ufumbuzi wa haraka juu ya kadhia ya kufungwa kwa benki ya FBME na namna ya kuwapatia haki zao waathirika wa benki hiyo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Hatua za kidiplomasia zinahitajika ili kulipatia ufumbuzi suala la haki za wananchi waliokuwa na akaunti kwenye benki iliyofungwa ya FBME. Aidha, Kamati inashauri Benki Kuu ya Tanzania kufanya kikao na wahanga hao ili kuwaeleza hatua iliyofikiwa katika ushughulikiaji wa kadhia yao ili warejeshe Imani kwa waathirika hao.
2. Ni busara Benki Kuu ya Tanzania ikaendelea na juhudi za kutoa elimu kwa wananchi juu ya alama za usalama kwenye noti zetu halali za Tanzania na mikakati mipya inahitajika ili kuepusha uingiaji wa noti bandia kenye mzunguko wa fedha nchini.
3. Ni wajibu wa Serikali kuu kuhakikisha nchi yetu inakua salama kwenye sekta ya fedha kwa kuhakikisha sheria zote zinazoongoza huduma ndogo za fedha (microfinance) zinaimarika na kuwaepusha wananchi na utapeli wa wajanja wachache.
4. Kutokana na tishio la uhalifu kupitia mashine za ATM, Kamati inashauri mashine zitakazonunuliwa ziwe maalum zinazozingatia usalama zaidi (risk management).

5. Kupitia shughuli zake, Kamati imebaini kuwa kufungwa kwa taasisi binafsi za kubadilishia fedha (bureau de change) kumepelekea vijana wengi kukosa ajira nchini. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuzipa vibali taasisi binafsi za kubadilishia fedha (bureau de change) zilizokidhi vigezo vilivyowekwa na kuziruhusu kutoa huduma hadi muda wa usiku ili kuwaondolea usumbufu wananchi wetu

## 2.7 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Ni benki ya Serikali iliyoanzishwa mwaka 1966 kwa mujibu wa sheria ya makampuni (Zanzibar Companies Decree, cap 153) na inatekeleza majukumu yake chini ya sheria ya makampuni nambari 15 ya mwaka 2013. Hadi kufikia tarehe 31/12/2021, PBZ ilikuwa na wafanyakazi 497 kati ya hao wanaume 274 na wanawake 223.
Hadi sasa, benki ina jumla ya matawi 16, Vituo 6 vya kutolea huduma, mashine 35 za kutolea fedha (ATM), maduka 6 ya kubadilishia fedha na mawakala 266 katika mikoa mbalimbali ya Tanzania.

Raslimali za benki ziliongezeka kwa asilimia 17, zilikadiriwa zifikie shilingi 846.56 bilioni ingawa zilivuka lengo na kufikia shilingi 995.96 bilioni. Ukuaji wa raslimali umechangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa mikopo. Asilimia 54 ya raslimali za benki hadi Disemba 2021 ni mikopo.

Mikopo ya benki imevuka lengo kwa asilimia 12 kutoka kiwango kilichokadiriwa cha shilingi 479.54 bilioni na kufikia shilingi 535.73 bilioni. Ongezeko la mikopo ya benki kwa kiwango kikubwa limesababishwa na kuongezeka kwa utoaji wa mikopo ya wafanyakazi wa sekta ya umma.

Amana za watejaziliongezeka na kuvuka lengo kwa asilimia 21 ya kiwango kilichokadiriwa cha shilingi 622.54 bilioni na zilifikia shilingi 755.27 bilioni.Amana ziliongezeka kutokana na kuongezeka kwa amana za muda maalum na amana za akiba ambazo zilifanyiwa maboresho kwa kuwalipa wanaowekeza faida ama riba kwa mujibu ya matakwa yao.

Faida kabla ya kodi zilifikia shilingi 24.860 bilioni ambazo ni pungufu kwa asilimia 22 ya kiwango kilichokadiriwa cha shilingi 31.850 bilioni.Kupungua kwa faida ya benki kunatokana na uwepo wa gharama za tengo (provision) za akaunti za PBZ zilioko katika mabenki mengine nje ya Tanzania.

## UKUSANYAJI MAPATO KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA (JULAI- DISEMBA 2021)

Kwa kipindi cha mwaka 2021, Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ) ilikadiriwa kukusanya mapato ya jumla yashilingi 96.76 bilioni lakini ilivuka lengo kwa asilimia moja (1) nakukusanya jumla ya shilingi 98.21 bilioni.Ukuaji wa mapato umechangiwa na ukuaji wa riba za mikopo kutokana na ukuaji wa utolewaji wa mikopo ya wafanyakazi na ile ya biashara.

## MATUMIZIJULAI HADI DISEMBA 2021

Matumizi ya benki yalifikia shilingi 73.35 bilioni, sawa na asilimia kumi na tatu (13) zaidi ya makadirio ya shilingi 64.91 bilioni. Hali hii ilisababishwa na ongezeko la gharama ya riba ya akaunti za muda maalum, akaunti hizi zimeongezeka hasa baada benki kuziongezea ubunifu wa huduma hiyo ambayo inamuwezesha mteja kupata malipo yake ya riba ama faidakila mwezi ama katika muda atakaochagua. Gharama nyengine zilizoongezeka ni za ukarabati na matengenezo ya vifaa na mifumo mbalimbali ya kibenki, gharama za ulinzi wa matawi na vituo vya kutolea huduma ambazo zimekuwa zinaongezeka kutokana na benki kuongeza huduma zake katika maeneo mbalimbali.Pia ongezeko la gharama ya jumla lilichangiwa na gharama ya tengo (provision) la raslimali nyengine (akaunti za benki ziliopo nje ya Tanzania).

## CHANGAMOTO

1. Baadhi ya taasisi za Serikali kuweka fedha kwenye benki nyengine jambo ambalo linapunguza wateja wa PBZ.

2. Sheria ya manunuzi inakwaza ufanisi wa manunuzi ya haraka kwa benki hii na kupelekea kudorora kwa maamuzi na kutomudu ushindani wa kibiashara.
3. PBZ ni benki ya kibiashara inayoshindana na mabenki mengine. Hivyo, uendeshwaji wake wa mfumo wa Idara kama Idara nyengine za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar unapelekea athari za kiutendaji na za kimaslahi. Benki hulazimika kufuata masharti ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ambayo ndiyo regulator wa benki za biashara na pia kufuata kanuni za Serikali kupitia Afisi ya Rais, Fedha na Mipango.
4. Kupungua kwa akiba za wateja kunakosababishwa na mzunguko mdogo wa fedha kutokana na maradhi ya UVIKO – 19 yaliyoikumba dunia.
5. Huduma dhaifu kwa wateja hupelekea kuhamia mabenki mengine yaliyopo nchini.
6. Kuchelewa kuingia kwenye mfumo wa bank insurance jambo ambalo linapelekea upotevu wa mapato kwa taasisi mbili za Serikali Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) kwa pamoja.
7. Kuchelewa kufanya maandalizi ya mifumo kunakoisababishia benki kushindwa kutekeleza majukumu makubwa ya kitaifa yakiwemo ya kuzihudumia fedha za ahueni ya UVICO – 19 ambazo Serikali imeshawishika kuzikabidhi kwa benki ya CRDB kutokana na utayari wake.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inauagiza uongozi pamoja na watendaji wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kutoa huduma bora zitakazowavutia wateja na kuwashawishi ili wasichukuliwe na mabenki mengine yaliyopo nchini. Kufanya hivyo kutatanua wigo wa benki hiyo na kulinda heshima yake kama ni benki pekee inayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100.
2. Ili kuiruhusu benki kujiendesha kibiashara, Kamati inaishauri Serikali kuupitia kwa makini muundo wake na kujiridhisha iwapo unaakisi malengo ya kuundwa

kwake. Kuendesha benki ya kibiahsara kwa mfumo wa Idara ni kikwazo kwa maendeleo ya benki yetu.

3. Kamati inashauri Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kuhakikisha inatengeneza faida nzuri kupitia matawi yake yote na kuiangalia kwa makini hisa ya asilimia 75% iliyowekezwa kwenye ununuzi wa benki ya jamii ya MUKOBA ya Iringa.
4. Kamati inashauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kuharakisha utoaji wa mikopo mara tu baada ya kukamilika kwa taratibu zilizopangwa na kuwajengea imani wananchi kuhusu uimara wa benki yao.
5. Huduma za Benki ya watu wa Zanzibar zinapaswa kuwa ni za haraka na zenye ufanisi wa hali ya juu ili kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya sekta ya fedha nchini. Sambamba na hilo, benki inawajibu wa kuajiri mtaalamu wa masuala ya Bank Insurance haraka iwezekanavyo ili kukidhi vigezo vya uanzishaji wa huduma hiyo.
6. Ili kuzitumia vyema fursa za kibiashara, Serikali haina budi kuiwezesha benki ya watu a Zanzibar kwa kuitengenezea mifumo itakayofanikisha majukumu yote makuu ya Kitaifa. Jambo hili litaipa heshima kubwa PBZ na kutengeneza faida nzuri.
7. Kamati inaiomba Wizara kupitia PBZ kuwapatia huduma maalum za afya Watendaji wa strong room kutokana na mazingira magumu ya kazi yanayohatarisha afya zao. Kadhalika, maslahi maalum yanayotokana na kazi yao yanapaswa kuandaliwa ili kuwatia moyo watendaji hao.

## 2.8 MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA (OFISI YA ZANZIBAR)

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imeundwa kwa sheria namba 11 ya mwaka 1995 na imeanza kazi rasmi mwezi wa Julai mwaka 1996 ikiwa na jukumu kuu la kusimamia ukusanyaji wa kodi na ada mbalimbali zinazotozwa na Serikali Kuu. Kwa upande wa Zanzibar, ofisi ya TRA inaongozwa na Naibu Kamishna na ina jumla ya Watendaji 167, kati yao wanawake 47 na 120 ni Wanaume.

Ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, TRA Ofisi ya Zanzibar inasimamia sheria zifuatazo:

- Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004
- Sheria ya Forodha ya Afrika Mashariki namba 1 ya mwaka 2004
- Sheria ya ongezeko la thamani (VAT) namba 4 ya mwaka 1998
- Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Cap. 147
- Sheria ya Kodi za Mafuta na Nishati namba 3 ya mwaka 1991
- Sheria ya Kodi ya Ufundi Stadi (SDL) namba 8 ya mwaka 2006
- Sheria ya Biashara namba 14 ya mwaka 2013.

Sekta kubwa ambazo zinachangia mapato yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika Ofisi ya Zanzibar ni utalii, mawasiliano, ujenzi, biashara, huduma za umma, huduma za fedha pamoja na sekta ya mafuta na gesi.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Mapato Tanzania Ofisi ya Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi413.07 bilioni kupitia Idara ya Forodha na Ushuru wa bidhaa na Idara ya Kodi za Ndani. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba2021, TRA Zanzibar imekusanya jumla ya shilingi165.519bilionidhidiyamakadirioyakukusanya shilingi 201.403 bilioni sawanaasilimia 82%ya makadirio.

## CHANGAMOTO

1. Kampuni nyingi za utalii nchini zimewasilisha taarifa ya kupata hasara katika biashara kwa mwaka huu ambapo sekta hiyo bado haijaimarika sana kutoka katika janga la UVIKO – 19 na hivyo kutowajibika kulipa kodi na kupelekea upungufu wa makusanyo.
2. Kupungua kwa viwango vya kodi ya PAYE kutokana na mwongozo wa Serikali.
3. Uchelewaji wa utatuzi wa migogoro ya kodi katika ngazi ya mahakama za kodi katika kesi zinazotokea baina ya Mamlaka ta Mapato Tanzania na walipa kodi mbali mbali.

4. Watumishi wapya wa Mamlaka ya Mapato Tanzania hawana ujuzi wa kutosha katika fani za utozaji wa kodi kwa kampuni zinazofanya kazi kati ya Zanzibar na nchi za nje (international taxation). Kasi ya kustaafu wataalamu wabobezi haiendani na kasi ya uajiri. HivyoTRA inakabiliwa na uhaba wa watendaji wenye ujuzi.
5. Ufinyu wa nafasi katika bandari ya Zanzibar unapelekea msongamano wa meli za mizigo zikitokea katika bandari ya Mombasa Kenya na Bandari ya Dar-es-salaam na kupelekea kupungua kwa kasi ya uteremshaji wa makontena na hivyo kuathiri mzunguko wa biashara na malipo ya kodi.
6. Mwamko mdogo wa ulipaji wa kodi kwa hiari baina ya wananchi.
7. Tofauti ya sera na Vipaumbele vya kodi baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania(SMT) zinasababisha ugumu wa kuweka uwiano katika matakwa ya kila Serikali katika usimamizi wa kodi.
8. Mishahara na marupurupu ya Wafanyakazi wa kigeni wenye taaluma mbali mbali wanaofanya kazi katika sekta mbali mbali za uchumi hailingani na uhalisia wa mishahara inayolipwa katika nchi wanazotoka katika taaluma husika.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Ili kuondoa mgongano wa mawazo miongoni mwa wananchi, ni vyema TRA ikajipanga kufanya utafiti wa namna ya kukusanya kodi kwa pamoja na kuweka vigezo maalum ili kumtambua mfanyabiashara mdogo na mkubwa.
2. Katika jitihada za kuongeza makusanyo ya kodi nchini, Kamati inashauri watumiye njia mbadala za uhamasishaji badala ya kutumia njia ya sasa ya kupitia kwa masheha pekee.
3. Kamati inaishauri Serikali kuanzisha bandari kavu katika maeneo mbalimbali nchini ili kuondoa msongamano wa meli za mizigo bandarini na kuepusha kupanda bei kwa mizigo hiyo inapoingia sokoni.

4. Taasisi za Serikali ziwajibike kufanya tax clearance kwa wakati na kwa usahihi zaidi kabla ya kufanya transfer kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato nchini.

## 2.9 BODI YA MAPATO ZANZIBAR (ZRB)

Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) ilianzishwa rasmi Septemba 1998 chini ya sheria Namba 7 ya mwaka 1996 ikiwa na dhima kuu ya kukusanya mapato ya ndani kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sambamba na hilo, bodi inawajibu wa kumshauri Waziri anaehusika na masuala ya fedha kuhusu maswala ya sera za fedha na kodi.

Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) imepewa uwakala wa kusimamia na kukusanya ada na kodi zilizokua zinasimamiwa na Taasisi nyengine nchini kama ada za leseni ya udereva, leseni za njia, usajili wa vyombo vya moto pamoja na kodi ya ardhi. Kamati iliarifiwa kuwa Bodi imeimarisha ukusanyaji wa mapato kwa kuanza kutumia mashine za kielektroniki.

### UKUSANYAJI WA MAPATO

Kwa kipindi cha Julai-Disemba 2021, jumla ya shilingi 263.80 bilioni zilikadiriwa kukusanywa ambapo makusanyo halisi ya kipindi hicho ni jumla ya shilingi 170.17 bilioni sawa na asilimia 64.51 ya makadirio.

Aidha, katika kipindi hicho ZRB ilikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 8.47 bilioni kutoka hazina ya Serikali, TRA na Mapato mengineyo ambapo jumla ya shilingi 7.87 bilioni ziliingizwa sawa na asilimia 92.92 ya makadirio.

## MATUMIZI HADI DISEMBA 2021

Kwa kipindi cha Julai-Disemba 2021, jumla ya shilingi 7.22 bilioni zilikadiriwa kutumiwa na Bodi ya Mapato Zanzibar ambapo hadi kufikia Disemba 2021, jumla ya shilingi 6.66 bilioni ziliingizwa na kutumika sawa na asilimia 92.29 ya makadirio.

## CHANGAMOTO

1. Ukwepaji mkubwa wa kodi ya ardhi kwa baadhi ya wawekezaji nchini ambapo Kamati imebaini kuwa miradi hubadilishwa mmiliki kila ikikaribia muda wa kuanza kulipa kodi hiyo jambo ambalo linaikosesha Serikali mapato.
2. Ukusanyaji wa kodi ya mahoteli *(hotel leavy)* umepungua kutokana na mfumo wa watalii kulipia katika nchi zao wanazotoka.
3. ZRB ina deni la Tsh. 8 bilioni kwa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO).
4. Mwamko mdogo wa wananchi juu ya suala zima la kudai risiti kila wanapofanya manunuzi hata baada ya kuanza matumizi ya mfumo wa kielektroniki (VFMS)
5. Kupungua kwa miradi mikubwa ya Serikali ambayo pia ilikua na mchango kwenye kodi.
6. Ingawa Serikali imeanzisha mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa kielektroniki, bado kuna wafanyabiashara wasio waaminifu ambao hawajaitikia wito huo na hawatumii mfumo huo kwa visingizio mbali mbali.
7. Kupungua kwa biashara za ndani ikiwemo matumizi ya mafuta na nishati, huduma za mawasiliano na usafiri nje ya nchi kutokana na kupungua kwa shughuli za kiutalii.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kutokana na mazingira halisi ya utendaji kwenye sehemu ya mitambo ya ZRB, Kamati inashauri mambo yafuatayo yafanyike:

i. Wizara iwapatiye mafunzo ya uhakika watendaji wa sehemu hii ili kuhakikisha mitambo iliyopo inadumu kwa muda mrefu na kulinufaisha Taifa letu.
ii. Hatua za tahadhari zichukuliwe ili kulinda afya za watendaji wa sehemu hii.
iii. Wizara iwapatiye watendaji wa eneo hili vivutio maalum ili kuwadhibiti wasirubuniwe na wakwepa kodi.

2. Kamati inawaomba Makatibu wakuu na Maafisa mas-uli wa taasisi za Serikali kuwasilishwa kwa wakati *withholding tax* kwenye Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB)ili kuongeza ufanisi wa taasisi hiyo.
3. Bodi iendelee na ukaguzi wa namna mashine za kielektroniki zinavyofanya kazi kutokana na ukweli kwamba mashine hizo ni mpya kwa wafanyabiashara wetu. Pia, usajili wa walipakodi wapya kwenye mfumo huo ni muhimu katika kuongeza mapato yetu.
4. Kufuatia madeni makubwa wanayodaiana ZECO na ZRB, Kamati inaiagiza ZRB kufanya mazungumzo na ZECO ili kulihakiki deni hilo na kuanza taratibu za kulipana ili kuendeleza mzunguko wa fedha nchini na kuziwezesha taasisi hizi kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## SEHEMU YA TATU

## AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

### 3. UTANGULIZI

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezajiina jumla ya Idara 8, Ofisi Kuu Pemba na taasisi 2 zinazojitegemea kama zifuatazo:-

### IDARA

1. Kamisheni ya Kazi
2. Ajira
3. Usalama na Afya Kazini
4. Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Wananchi Kiuchumi
5. Maendeleo ya Vyama vya Ushirika
6. Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi
7. Uendeshaji na Utumishi
8. Mipango, Sera na Utafiti na
9. Ofisi Kuu Pemba

### TAASISI ZINAZOJITEGEMEA

1. Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA)
2. Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEF)

### 3.1 UKUSANYAJI MAPATO KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA (JULAI- DISEMBA 2021)

Afisi katika kipindi cha Julai – Disemba, 2021 ilitarajiwa kukusanya Mapato ya jumla ya Shilingi 1,463,126,000 bilioni lakini imefanikiwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi 654,982,926 milioni sawa na asilimia 45 ya lengo kutokana na Ada za

Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi, Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi

## 3.2 MATUMIZI JULAI HADI DISEMBA 2021

### 3.2.1 FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

Kwa Kipindi cha Julai – Disemba 2021 Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia fungu A07 (Kazi na Uwezeshaji) iliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi 3,844,937,795 bilioni. Kati ya fedha hizo, Shilingi 877,236,820 milioni ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Usimamizi wa Sheria za Kazi, Ukaguzi Kazi na Kazi za Staha kwa wote,Shilingi 845,650,477 milioni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi naShilingi 2,122,050,498 bilionikwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Kiuhalisia, jumla ya shilingi 2,294,605,336 bilioni ziliiingizwa na kutumika sawa na asilimia 60 ya makadirio.

### 3.2.2 FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

Kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwezeshaji) Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezajiiliidhinishiwa kutumia jumla ya Shilingi 1427,912,000 bilioni kwa kipindi cha Julai – Disemba 2021. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,261,447,000 bilioni ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Kuimarisha Uwekezaji na Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi na Shilingi 166,465,000 milioni ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Kiuhalisia jumla ya shilingi 707,636,115 bilioni sawa na asilimia 50 ya makadirio.

## 3.3 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA)

Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar ni Taasisi ya Serikali inayofanyakazi chini ya Sheria ya Mamlaka ya kukuza na kulinda Uwekezaji Zanzibar Na. 14, 2018. Jukumu la

msingi la Mamlaka hii ni kutekeleza sera na Sheria ya Uwekezaji kikamilifu kwa nia ya kuwavutia wawekezaji wenye tija kwa manufaa ya nchi na wananchi wake.

Serikali, kupitia Mamlaka hii imeelekeza nguvu zake katika kutangaza na kusimamia Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2008 katika sekta zote zinazohusika. Aidha, mkazo maalum umewekwa kwenye uimarishaji wa uchumi wa buluu ikizingatiwa kuwa jiografia ya Zanzibar ni visiwa na ina uwanja mpana wa kuimarisha sekta hiyo.

## CHANGAMOTO

1. Mamlaka kutokua na maeneo yanayotosheleza kwa ajili ya uwekezaji (Land Bank) ambapo maeneo makubwa yaliotengwa kwa ajili ya uwekezaji yameshakodishwa kwa ajili ya miradi mbali mbali.

2. Baadhi ya maafisa wa Wizara na Taasisi zinazojihusisha na program ya '*one stop centre*' hawana mamlaka ya kufanya maamuzi ya moja kwa moja na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa baadhi ya vibali.
3. Kuna changamoto kubwa ya miundombinu ya maeneo huru ya uwekezaji ambapo kuna uhaba wa upatikanaji wa maji, umeme na kuwepo kwa barabara zisizokua na kiwango kinachohitajika.

4. Jengo la Ofisi la ZIPA halina hadhi ya mamlaka husika, halina mvuto kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

5. Kukosekana kwa usafiri wa kutosha wa kuenda kutembelea na kukagua maeneo ya Uwekezaji.

6. Baadhi ya miradi ambayo imepitishwa na ZIPA hususan inayohusu uzalishaji wa bidhaa inakabiliwa na changamoto kubwa za kibiashara zinazotishia uhai wake.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Serikali kuyarudisha maeneo huru ya uwekezaji ambayo wawekezaji waliokabidhiwa wameshindwa kuyaendeleza ili kuengeza maeneo ambayo yapo tayari kwa uwekezaji (*Land bank).*

2. Ni vyema Serikali kuijengea Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar Jengo ambalo litaendana na hadhi ya Taasisi hiyo na kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini.

3. Ili tuyafikiye malengo ya Serikali yetu ya awamu ya nane yakuwainua wananchi kiuchumi kupitia uwekezaji, Kamati inashauri Taasisi za Serikali kuwa na nia ya dhati katika utendaji wao na kuacha tabia ya kutupiana majukumu baina ya Taasisi moja na nyengine.

4. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara husika kuwapa mamlaka maafisa wanaohusiana na dhana ya *'One Stop Centre'* kufanya maamuzi yote yanayohusiana na shughuli mbali mbali za taasisi.

5. Kamati inashauri Serikali kutotoa kibali cha *'Soft Opening'* mpaka mradi husika ufike asilimia 70 ya ukamilifu wake kwani kumejitokeza wawekezaji wasio waaminifu wanaoomba kufungua biashara zao mapema kwa nia ya kukwepa kodi ya Serikali.

6. Ni dhahiri kuwa suala la ukaguzi ni muhimu katika kuhakikisha utekelezaji wa Sera na Sheria zinazoongoza uwekezaji nchini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuipatia vyombo vya usafiri ZIPA ili iweze kuyatembelea na kuyakagua maeneo yao maalum ya Uwekezaji.

7. Kamati imesikitishwa na ukoseshaji wa ajira kwa Wazanzibari katika miradi iliyo chini ya ZIPA na kushauri kuwa taratibu za kisheria zifuatwe na kupatiwa wazalendo ajira ikiwa ni hatua muhimu katika kulifikia lengo letu la ajira nchini.

8. Kamati inaitaka Wizara kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya eneo huru la Micheweni na kuhakikisha umeme, maji, barabara na huduma za mawasiliano vinapatikana kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji nchini. Aidha, Kamati inasisitiza haja ya Mheshimiwa Waziri kufanyamazungumzo maalum na Mheshimiwa Rais ili kumuarifu hali ya maeneo yetu ya uwekezaji na kuandaa mikakati ya pamoja ya kuyafanya maeneo hayo yawavutiye wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

9. Kwa vile hali ya wawekezaji wa viwanda vya uzalishaji ni mbaya na wanakabiliwa na changamoto za kibiashara ambazo ziko nje ya uwezo wao, ni vyema Serikali Kuu ikaingilia kati ili kuihami hali hii na kurejesha ajira za vijana wetu kwenye sekta ya viwanda.

10. Kamati imearifiwa kuwepo kwa timu ndani ya ZIPA ambayo inafanya mapitio ya Mpango Mkuu (Master Plan) ya eneo huru la uwekezaji Fumba na inashauri shughuli hiyo ifanyike ndani ya wakati uliopangwa na kwa ufanisi.

11. Kamati imearifiwa kuwa bado taasisi hii inapokea ruzuku kutoka Serikalini. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo ili kuongeza mapato na hatimae itoke katika usimamizi wa Serikali kifedha.

12. Katika uwekezaji wa hoteli uliofanywa ndani ya visiwa vyetu, ni wazi kua hoteli nyingi sana zinafanana kimuundo mpaka kihuduma. Kamati inashauri ZIPA kutoa miongozo katika uwekezaji wa ufukweni hususani katika sekta za Hoteli ili zitofautiane dhana, miundo, huduma na kuongeza mvuto wa uwekezaji, biashara na utalii.

## 3.4 IDARA YA USHIRIKIANO BAINA YASEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI (PPP)

Idara ya Ushirikiano Baina ya Serikali na Sekta Binafsi ni Idara inayojishughulisha na makubaliano ya kimkataba baina ya Sekta Umma na Sekta ya Binafsi, ambapo Sekta Binafsi inatoa huduma kwa niaba ya Serikali. Makubaliano hayo ni baina ya Serikali (Taasisi zenye miradi) pamoja na Mwekezaji binafsi kwa kuratibiwa na Idara ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Miradi ya mfumo wa PPP ni miradi ya muda mrefu inayohususha ujenzi wa miundombinu na utoaji wa huduma ambapo awali huduma hizo zilikua zikitolewa na Serikali.

Kamati iliarifiwa kuwa Wizara inaandaa marekebisho ya sheria ya PPP kwa nia ya kuitoa PPP katika Afisi ya Rais, Fedha na Mipango na kuiweka chini ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ambapo ndio pahala stahiki kwa ajili ya utendaji bora wa miradi yake.

## CHANGAMOTO

i. Miradi iliyoibuliwa chini ya utaratibu huu ni mingi lakini hukosa approval na hivyo hubakia kwenye mchakato tu bila ya kutakelezwa.
ii. Baadhi ya miradi ya PPP Zanzibar imekamilika uandaaji wake lakini imekwama kutokana na kukosa saini ya Tanzania Bara. Kwa mfano mradi wa solar.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

i. Kamati inashauri Serikali kuitumia Idara hii kuhamasisha uwekezaji wa miradi mbali mbali kwa manufaa ya Wazanzibari.
ii. Kamati inashauri Idara kutoa elimu kwa jamii juu ya faida za mikataba ya PPP
iii. Ili kufikia malengo yaliyopangwa, iko haja kwa PPP kufanya kazi kikamilifu kwa mujibu wa sheria.

iv. Kamati inashauri Idara kuwazingatia wale walioibua dhana ya mradi itakayotekelezwa kwa njia ya PPP na kuwapatia asilimia fulani ya tija miradi hiyo ili kuhamasisha jamii juu ya kuibua miradi mbalimbali.

## 3.5 IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA SHUGHULI ZA WAZANZIBARI WALIOPO NCHI ZA NJE

Kamati ilipata fursa ya kukutana na Uongozi wa Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa shughuli za Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi na kupokea taarifa ya utendaji wa shughuli zao.

### CHANGAMOTO

1. Ushiriki wa Zanzibar katika masuala ya mbali mbali ya kikanda na kimataifa ni mdogo sana
2. Mipangilio yote ya kuratibu mikutano ya kikanda na kimataifa hufanywa na Wizara husika Tanzania Bara bila ya kushirikishwa Wizara husika Zanzibar au kupewa taarifa mwishoni kabisa hali inayofanya kukosekana kwa matayarisho bora ya kuiwakilisha Zanzibar katika vikao mbali mbali ya kikanda na kimataifa.
3. Idara inakabiliwa na uhaba wa bajeti ya kuratibu safari au shughuli zake nje ya nchi
4. Wafanyakazi wa Idara hii wamekua wakipangiwa Zaidi kazi za kiitifaki licha ya wafanyakazi hao kua na taaluma ya mambo mbali mbali
5. Wizara inayohusiana na mambo ya nje ya Muungano hua inatoa mialiko kwa taasisi mbali mbali ndani nan je ya nchi bila ya kufata taratibu za kushauriana na kuitaarifu Idara
6. Kuna ufahamu mdogo sana wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi kwenye masuala mazima ya Sera na Sheria za *'Diaspora'*

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

i. Kamati inashauri Idara kufanya juhudi za ziada kuwahamasisha Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi hususani wale wenye uwezo mkubwa sana wa kifedha kuja kuwekeza nyumbani.
ii. Kamati inashauri Serikali kuwapa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi *(Diaspora)* kupewa upendeleo maalum pindi tu watapokuja kutembea nyumbani ili na wao wajisikie wanakuja nyumbani na sio ugenini.
iii. Kamati inashauri Serikali kuweka fungu maalum la fedha la kurahisisha uratibu wa masuala mazima ya kikanda na kimataifa
iv. Kamati inashauri Serikali kuweka utaratibu maalum wa kuwahamasisha *'Diaspora'* kutuma fedha ndani ya nchi katika utaratibu unaotambuliwa na Serikali ili kuengeza mapato yanayotokana na kodi ya fedha inayotumwa kutoka nje

## 3.6 KAMISHENI YA KAZI

Kamisheni ya Kazi ipo chin ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na imeanzishwa chini ya Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2005. Jukumu hasa la Kamisheni ya Kazi ni kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi katika sekta binafsi kwa hapa Zanzibar. Kamisheni ya Kazi ina jukumu la kufanya ukaguzi kazi kwa Taasisi zote za sekta binafsi na kusimamia Ajira za wafanyakazi wa kigeni, kuthibitisha mikataba ya wafanyakazi wazalendo na wageni na kusimamia uimara wa mahusiano mema kati ya waajiri na waajiriwa katika sehemu ya kazi.

## CHANGAMOTO

1. Kamisheni ina uhaba wa wataalamu ambapo kuna maeneo ambayo yanahitaji wataalamu wenye taaluma maalum na ya hali ya juu
2. Kuna uhaba wa maafisa kazi na hii inapelekea kutofikiwa kwa taasisi ndani ya muda uliopangwa
3. Ugumu wa kufanya kazi kwa ufanisi kutokana na uhaba wa vyombo vya usafiri
4. Kutokua na utaratibu mzuri wa uwekaji wa taarifa *(Database System)*

5. Kamisheni haina jengo la kudumu la kufanyia kazi. Aidha, nafasi ndani ya ofisi ya sasa ni ndogo sana kutokana na ukubwa wa Idara zake.
6. Ni busra Kamisheni ya Kazi ikaandaa mwongozo wa ajira za muda mfupi ambao utafuatwa na taasisi zote nchini. Kitendo hichi kitawafanya vijana wetu kuwa na uhakika wa ajira kwa muda wa mkataba husika. Aidha, Kamisheni ipewe mamlaka ya kufuatilia ajira za taasisi binafsi ili kuhakikisha miongozo ya Serikali inafuatwa katika suala la uajiri.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri kuchukuliwa hatua za Kisheria Taasisi ambazo bado zinatoa mishahara chini ya kima kilichoekwa na Serikali kwani kitendo hicho kinawadhalilisha wafanyakazi hao na familia zao.
2. Kamati inashauri Kamisheni kuingiza mafunzo ya kazi *(Refresher courses)* kwa watendani wote katika mpango wake wa ofisi
3. Kamati inaishauri Serikali kuliangalia suala zima la vyombo vya usafiri kwa ajili ya ukaguzi wa maeneo ya kazi ili kurahisisha shughuli za Kamisheni.
4. Kamati inaishauri Serikali kuiunga mkono Kamisheni katika suala zima la kutumia teknolojia katika utunzaji wa taarifa *(Database system).*

## 3.7 MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni Taasisi ya Utoaji wa Huduma za Mitaji kwa Wajasiriamali Wadogo ili waanzishe na kuendeleza Miradi yao ya Kiuchumi itayowapatia kipato cha kujikimu kwa maisha yao ya kila siku na ya familia zao.Kwa kipindi cha Julai - Disemba, 2021Mfuko umetoa mikopo 248 (Unguja 136 na Pemba 112) yenye jumla ya Shilingi 210,050,000 milioni.

Kamati iliarifiwa kuwa mfuko ulishiriki kikamilifu katika kufanikisha maonesho ya wajasiriamali wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yaliyofanyika Mwanza Tanzania. Jumla ya wajasiriamali 18 kati ya 46 wa Zanzibar walioshiriki maonesho hayo ni wateja wa Mfuko. Kupitia maonesho hayo wajasiriamali wetu wamepata uzoefu na wamejifunza kutoka miongoni mwao. Pia, wamepata fursa ya kubadilishana bidhaa katika nchi tofauti

zilizoshiriki, jambo ambalo limepelekea kuzitangaza bidhaa zao na kujenga ukaribu baina ya wajasiriamali wa ndani na nje ya Tanzania.

## CHANGAMOTO

1. Wajasiriamali walio wengi hawana muono wa mbali jambo ambalo hupelekea kutotumia kikamilifu fursa za kukua kibiashara zinazotokea kwa upande wao. Baadhi yao huridhika kwa kipato kidogo tu na kuendelea kuwa duni kimaisha wao na familia zao.
2. Taarifa sahihi juu ya fursa za mikopo kwa kiasi kikubwa haziwafikii wajasiriamali wetu na hivyo wanashindwa kuzitumia kwa maendeleo ya shughuli zao.
3. Sera ya biashara huria inawaumiza wazalishaji wadogo wadogo kwani baadhi yao huzalisha na kuuza kwa bei ya chini ilhali bidhaa ileile inauzwa kwa bei ya juu na mtu wa kati sokoni.
4. Mashirikiano madogo baina ya wawezeshaji na sekta wanazozifanyia kazi wajasiriamali hupelekea kukosa matokeo mazuri kwenye shughuli zao.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri vikundi vinavyolengwa kuwezeshwa kiuchumi visikabidhiwe fedha taslim bali vipatiwe nyenzo na vifaa vya uzalishaji kwani mara nyingi fedha hizo huwa hazitoshi kwa ajili ya kutekeleza miradi husika.
2. Ni vyema Serikali ikaweka utaratibu maalum utakaowanufaisha mzalishaji na mnunuzi wa jumla bila ya kuwaathiri wananchi ambao ndio wanunuzi.
3. Changamoto kuu ya wajasiriamali wetu ni ukosefu wa vifungashio vinavyokwenda na wakati. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kulivalia njuga suala hilo kwani limekua ni la muda mrefu sasa na linawakosesha soko wajasiriamali wetu.
4. Ili kutimiza azma ya Serikali ya awamu ya nane ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, Kamati inashauri mfuko wa uwezeshaji ushirikiane kikamilifu na sekta

husika ili kuwapatia wajasiriamali wetu nyenzo na utaalamu na hatimaye kuyafikia malengo yetu.

5. Uzalishaji wa bidhaa zinazohitajika kwa wingi uimarishwe ili wajasiriamali wetu waweze kukidhi mahitaji yetu ya ndani na oda zinazotoka nje ya nchi.

### 3.8 MRADI WA PENNYROYAL

Penny Royal ni mradi wa uwekezaji wa 'Real Estate' ambao umeanzishwa kwenye kijiji cha Mbuyu Tende katika Jimbo la Kijini, Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja. Jumla ya hekta 411.92 zinakusudiwa kutumika kwenye mradi huo mkubwa utakaohusisha ujenzi wa nyumba za makaazi, sehemu za kupumzikia, hoteli za kitalii na sehemu za michezo na kugharimu Dola za Kimarekani 1.6 bilioni sawa na shilingi za Kitanzania 3.376 Trilioni na kutoa ajira kwa vijana 40,000 mara baada ya kukamilika kwake. Mradi huo ulisajiliwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar ya mwaka 2004, naulianza mwaka 2011 kwa kuomba vibali Serikalini. Mradi umeidhinishwa kwenye miradi ya kimkakati '*Strategic Investment Project*' mnamo mwaka 2017 mara baada ya marekebisho ya sheria ya ZIPA iliyoingiza kifungu hiki. Mradi ulipatiwa umeme wa 5MG (Mega Watts) ambao unatosheleza kwa matumizi ya awali kabla ya kuanzisha umeme wa aina nyengine katika siku za usoni. Mnamo mwezi wa April 2018, mradi ulifanikiwa kupata hati ya matumizi ya ardhi (land lease) ya miaka 99 kwa mujibu wa sheria, ambapo Hati hiyo inampa fursa mwekezaji huyo kukopa katika Taasisi kubwa za fedha ndani na nje ya nchi. Mradi ulifanikiwa kupata kibali cha uwekezaji katika eneo la baharini (marina) mwezi Mei 2019.

Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi iliarifiwa kuwa mradi huo haukufanikiwa kufikia malengo yake kutokana na wataalamu kushindwa kubakia nchini kutokana na UVIKO - 19. Kamati imebaini kuwa ujenzi unaoendelea kwenye eneo la mradi huo haujahusisha mtaalamu wa kigeni na hivyo UVIKO - 19 haikua kizuwizi cha udororaji wake.

Aidha, Kamati haikuridhishwa na maendeleo ya Mradi huo ambapo dhana halisi ya Mradi huo haijatekelezwa na hadi wakati Kamati ilipotembelea mradi huo mwezi Januari, 2021 ni jumla ya Hekta 4.9 tu ndizo zilizotumika katika kufanya ujenzi kati ya Hekta 411.92 alizopatiwa mwekezaji.

## CHANGAMOTO

1. Mwekezaji amekua na khulka ya kubadilisha dhana ya mradi mara kwa mara jambo ambalo linapelekea upotevu wa kodi za Serikali kwani mabadiliko hayo hufanywa kila ikikaribia mwisho wa muda wa msamaha wa kodi (*tax holiday).*
2. Mkataba wa matumizi ya ardhi wa mwaka 2014 uliainisha ujenzi wa barabara kutoka Mwangaseki kupitia Kijini mpaka Muyuni eneo ambalo Kamati haikulitambua katika maeneo ya mradi na badala yake eneo la Kiashangwe ndilo lililofahamika.
3. Kupatikanika kwa Hati ya Matumizi ya Ardhi ya Hekta 411.92 kwa Mradi huo kinyume na taratibu ambapo ZIPA inatambua Hekta 162.34
4. Mkandarasi wa Mradi huo kutopewa '*Full Contract*', jambo ambalo ni kinyume na taratibu za ujenzi ambapo mkandarasi huyo amekua akiletewa tu vifaa vya ujenzi na mwekezaji wa mradi huo na jukumu lake yeye ni kujenga tu. Hali hii imepelekea ujenzi kuchukua muda mrefu sana.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Sekta ya ujenzi nchini imepata maendeleo makubwa na wataalamu wazawa wana uwezo wa kufanya shughuli nyingi. Hivyo, Serikali iandae utaratibu wa kisheria utakaowapatia fursa wataalamu wetu kupewa *full package* kwenye miradi wanayoisimamia badala ya kukabidhiwa kazi nusu nusu. Kadhalika, kampuni za

wazawa hazina uwezo mkubwa kifedha na kupelekea kushindwa kuingia kwenye ushindani wa kimataifa (*international tender*) hivyo, ni wajibu wa Serikali kuzinyanyua kampuni hizo kwa kuzipatia mikopo nafuu ili ziweze kukua na kuajiri vijana wengi zaidi.

2. Kutokana na udanganyifu mkubwa unaofanywa na mwekezaji wa mradi wa Penny Royal katika suala la ukwepaji wa kodi ambayo inakadiriwa kua Zaidi ya 4.5 bilioni, Kamati inapendekeza mradi huo ufutwe na Ardhi yote Pamoja na ile Ardhi ya baharini irudishwe Serikalini.

3. Kutokana na mradi kutumia hekta 4.9 kati ya hekta 411.92, Kamati inapendekeza eneo hilo litafutiwe wawekezaji wengine waliokua makini ambao wataliendeleza kwa manufaa ya Taifa.

4. Kamati inapendekeza mwekezaji kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kuudharau Muhimili wa Baraza kwa kupuuza maagizo ya Kamati ya Uchumi Pamoja na kutoa vitisho mbali mbali kwa Wajumbe wa Kamati hiyo.

5. Kamati inashauri utoaji wa maeneo ya uwekezaji ya baharini usitishwe kutokana na athari za kimazingira ambazo bado hazijapatiwa ufumbuzi.

6. Kutokana na malalamiko ya mwekezaji kua mradi huu hauwezi kumletea tija kwa kutozingatiwa maslahi ya mnunuzi wa nyumba hizo (*buyer's benefits*), Kamati inaishauri Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuwapa kazi maalum wataalamu wa ZIPA kufanya uchambuzi wa kitaalamu (*due diligence*) ili kujiridhisha ni faida gani itakayopatikana kwa nchi yetu iwapo tutaondoa kodi zote zinazotokana na mauzo ya nyumba hizo kwa mujibu wa matakwa ya mwekezaji.

7. Kamati inashauri wawekezaji wa miradi ya kimkakati kwenye sekta ya *real estate, w*anapoitumia fursa ya misamaha ya vifaa vya ujenzi, wawasilishe nyaraka zote zinazohusiana na utoaji wa vifaa hivyo katika Mamlaka ya Ukuzaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) ili kujiridhisha juu ya usahihi wa vifaa vinavyoingizwa.

8. Kamati inashauri kandarasi zote zinazohusu miradi mikubwa ya Serikali kuweka sharti la kumuambatanisha mtaalamu mzawa kila wanapowapa tenda wataalamu wa kigeni kwa yale mambo ambayo yako nje ya uwezo wa wakandarasi wazawa. Kufanya hivyo kutapelekea kujifunza kwa haraka na kukuza utaalamu wao.

9. Serikali isitishe na kufuta cheti cha uwekezaji kilichotolewa kwa mwekezaji wa mradi huu kwa mujibu wa kifungu cha 25(1) cha sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar (Na. 14, 2018) kutokana na ukweli kwamba mwekezaji huyu ameshindwa kuanza mradi kwa miaka mingi tangu alipopewa nyaraka zote za kisheria. Hatua hii ni muhimu katika kutimiza azma ya kuwapatia ardhi wawekezaji waliojiandaa na uwekezaji kwa wakati ili kuwekeza nchini na kuzalisha ajira kwa vijana wetu na kuinua pato la Taifa letu.

### 3.9 MRADI WA BAREFOOT

Mradi wa nishati mbadala ya umeme wa jua ambao umeanzishwa nchini mwaka 2015 kwa ajili ya kuwapatia umeme wananchi masikini ambao hawana uwezo wa kugharamia huduma ya umeme wa kawaida. Mradi umeanzisha kituo maalumu cha mafunzo (barefoot college) kilichopo Kinyasini Unguja ambacho kwa mujibu wa takwimu za Umoja wa Mataifa ni kati ya vituo 20 bora vya aina hiyo duniani. Mradi unatekelezwa pia kwa upande wa Pemba ambapoumeanza rasmi mwaka 2017 katika kijiji chaMakoongwe baada ya akinamama watatu kumaliza mafunzo yao ya uhandisi wa umeme wa juakatika chuo cha Barefoot Zanzibar kilichopo kaskazini Unguja.Kijiji cha Makoongwe kinajumla ya watendaji 8 kati yao 3 ni wahandisi wa umeme wa jua na 5 ni kamati saidizi kwa kazindogo ndogo zinazohusiana na mradi wa umeme wa jua.

Mbali na huduma hiyo ya umeme wa jua, kituo pia kinawapatia akinamama ujuzi wa shughuli mbali mbali za biashara ikiwemo mafunzo ya ufugaji wa nyuki na ushoni.

## CHANGAMOTO

1. Upungufu kwa kipato cha Mradi kila Mwaka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kupatikana kwa huduma ya umeme wa kawaida kwenye vijiji mbalimbali nchini hadi kufikia hatua ya kukosekana kabisa fedha za kuwalipa solar mamas kwa ajili ya kazi zao. Kwa mfano katika kijiji cha Makoongwe, hadi kufikia mwezi Agosti 2021, mradi ulifanikiwa kupachika Solar 50 tu na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 36,000 tu kati ya shilingi 2,400,000 za makadirio.
2. Ufinyu wa bajeti unaopelekea akinamama wanaomaliza mafunzo kubaki bila ya kupatiwa nyenzo za kufanyia kazi kwa muda mrefu.
3. Upeo wa mradi bado ni mdogo ambapo sola zinazotolewa zina uwezo wa taa nne tu ambazo hazilingani na matumizi halisi ya nyumbani kwa sasa.
4. Kamati imearifiwa kuwepo kwa Imani kwa wananchi kua Solar zimeletwa na Serikali kwa ajili ya Wananchi, hali inayosababisha ukosefu wa malipo ya solar hizo.
5. Ukosefu wa ofisi ambayo itatumika kama sehemu ya kuhifadhi solar hizo pamoja na vifaa vyake kwa kijiji cha Makoongwe.
6. Uelewa mdogo wa wanajamii juu ya umuhimu wa mradi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri kujikita katika kutoa elimu kwa wananchi ili kujua faida mbali mbali zinazotokana na Mradi huu na kusaidia kuulinda na kuuimarisha mradi huo.
2. Ni wajibu wa Serikali kukitunza na kukiendeleza kituo hiki cha mafunzo ili kiwe chachu ya mafanikio kwa akinamama ambao ndio tegemeo kwa familia zao.
3. Mradi utafute namna ya kushirikiana na Shirika la Umeme Zanzibar ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

## 3.10 ENEO LA VIWANDA - CHAMANANGWE

Kamati ya Uchumi ilitembelea kiwanda cha Maji cha AMOS INDUSTRIAL LTD kilichopo Chamanangwe. Kiwanda hicho kimeanzishwa baada ya kuitikia wito wa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambae anania ya kukifungua kisiwa cha Pemba kiuchumi na Zanzibar yote kwa ujumla.Kiwanda hicho kipo kwenye hatua za mwisho ili kuanza shughuli za uzalishaji wa maji na baadae soko litakaporuhusu kuanza kuzalisha vinywaji baridi hii ni kutokana na kuwepo kwa rasimali matunda kwa wingi haswa mabungo na embe katika kisiwa cha Pemba.Gharama za ujenzi wa kiwanda hicho,ufungaji wa mashine za uzalishaji pamoja na mtaji wao waliowekeza hadi sasa ni Dola za kimarekani 500,000 na inategemewa endapo kiwanda kitakapomaliza kitaweza kuajiri vijana wapatao elfu 50.

### CHANGAMOTO

1. Kamati imebaini kiwanda kutokua na kifaa cha kupima tarehe ya mwisho ya matumizi (expired date) ya bidhaaa.
2. Kamati imebaini kuwa kiwanda kina kisima kimoja tu cha uzalishaji maji hali ambayo inaweza kuleta uzoroteshaji wa huduma pindi maji yakipungua.
3. Kamati imebaini muekezaji huyo hakupatiwa ushauri elekezi kutoka kwa watu wa ZAWA kwani kwenye biashara ya uzalishaji wa maji uzoefu umeonesha viwanda vingi havitumii visima kama ndio chanzo kikuu cha upatikanaji wa malighafi maji.
4. Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto ya soko la kuuzia bidhaa hizo hususan watakapotaka kuingia kwenye soko la Tanzania Bara.

### MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiagiza Serikali pamoja na Mwekezaji huyo pindi uzalishaji utakapoanza basi kuhakikishaji wanaopewa kipaumbele cha ajira ni wakaazi wa eneo la chamanangwe.

2. Kamati inamuagiza Mwekezaji huyo pindi anapoanza uzalishaji basi ajitahidi kuweka huduma yoyote ya kijamii karibu na eneo hilo ili wanachi waweze kunufaika na mradi wa uwekezaji.

## SEHEMU YA NNE

## WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### 4. UTANGULIZI

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Idara sita na taasisi nne zinazojitegemea kama ifuatavyo:

### IDARA

i. Uendeshaji na Utumishi
ii. Mipango, Sera na Utafiti
iii. Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Ukijumuisha Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi)
iv. Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini
v. Hifadhi za Baharini
vi. Afisi ya Afisa Mdhamini – Pemba

### TAASISI

i. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Bahari;
ii. Kampuni ya Uvuvi;
iii. Kampuni ya Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (Zanzibar Petroleum Development Company);
iv. Mamlaka ya Kudhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (Zanzibar Petroleum Development Authority)

### 4.1 UKUSANYAJI MAPATO KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA (JULAI- DISEMBA 2021)

Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2021, Wizara ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,418,118,000 milioni ambapo ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 623,389,989 milioni sawa na asilimia 43.9 ya makadirio.

## 4.2 MATUMIZIJULAI HADI DISEMBA 2021

Kwa kipindi chaJulai hadi Disemba 2021, Wizara pamoja na taasisi zake zote iliingiziwa na kutumia jumla ya shilingi 3,246,091,429 bilioni.

## 4.3 PROGRAMU YA UVIKO - 19

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2021 imepatiwa jumla ya shilingi36.5 bilioni kutokana na fedha za ahueni ya UVIKO - 19, kwa ajili ya kuwawezesha wadau wa sekta ya Uvuvi na Ufugaji wa mazao ya Baharini. Kamati imearifiwa kuwa, Wizara imesaini jumla ya mikataba kumi na mbili (12) kupitia Kampuni saba (7) katika mchakato wa kufanya matumizi sahihi ya fedha hizo kama ifuatavyo:

a) Mikataba ya kampuni tano (5) za kutengeneza boti 300 za Uvuvi zenye urefu wa mita saba (7) ambapo kila boti moja itagharimu Dola za Marekani U$D 10,580 sawa na shilingi24.3Milioni. Hivyo boti zote 300 kwa ujumla zitagharimu jumla ya shilingi 7.3 Bilioni.

b) Mikataba ya kampuni nne (4) za kutengeneza boti 277 za Uvuvi zenye urefu wa mita nane (8) ambapo kila boti moja itagharimu Dola za Marekani U$D 13,800 sawa na shilingi 31,740,000milioni. Hivyo boti 277 kwa ujumla zitagharimu jumla ya shilingi 8.79 bilioni.

c) Kampuni moja imepatiwa mkataba wa kuipatia Wizara vifaa vya wakulima wa mwani vikiwemo tai tai na kamba za aina zote zinazohitajika katika ukulima wa mwani. Aidha, wakulima wa mwani 5000 watapatiwa vifaa hivyo vyenye jumla ya shilingi 1,587,600,000 bilioni.

d) Kampuni moja imepatiwa mikataba miwili inayohusiana na Ujenzi wa Mabwawa 100 ya Ufugaji wa majongoo bahari yenye thamani ya shilingi 465,727,000 milioni na

mkataba wa Ujenzi wa Mabwawa 60 ya ufugaji wa kaa kwa Unguja na pemba wenye thamani ya shilingi 264,270,000 milioni.

## CHANGAMOTO ZA WIZARA KWA UJUMLA

1. Baadhi ya ofisi ndani ya jengo kuna vitengo Zaidi ya viwili, hali inayopunguza ufanisi wa kazi.
2. Ofisi ya masjala ya uchumi wa buluu haina computer hata moja. Aidha wizara nzima ina uhaba wa vitendea kazi.
3. Utaratibu wa kuligawa Jengo hili kwa wizara tatu zinazotumia pamoja haukuipendeza Kamati wakati ilipotembelea eneo hilo.
4. Data room ya ZPDC ni ndogo. Wizara ichukue hatua za kutafuta chumba kikubwa Zaidi ili kukidhi mahitaji ya eneo hili.
5. Work centre ya ZPRA ina computer 2 na wafanyakazi wane. Ili kupata ufanisi wa kazi kamati inashauri kila mfanyakazi awe na computer yake. Halkadhalika vifaa tofauti vya ofisi vinakosekana ndani ya work centre hiyo kama vile printers etc, Hali hii inasikitisha ukizingatia unyeti wa kitengo hicho.
6. Mafunzo machache kwa watumishi wa ZPRA na ZPDC kuhusu mafuta na gesi .
7. Kamati imearifiwa kuwepo kwa uhaba mkubwa wa *Geophysicist* wanaohitajika na ZPRA.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiagiza Wizara kuchukua hatua stahiki katika kufanikisha shughuli ya kumtafuta *Geophysicist* anaehitajika na ZPRA
2. Wizara haina budi kutekeleza wajibu wake wa kuzipatia vifaa taasisi zake zilizomo ndani ya Ofisi ikiwemo taasisi za ZPDC na ZPRA

3. Sheria ya mafuta na gesi No. 6 ya 2016 inaitaka Kampuni ya ZPDC kuwasilisha mapato yote yanayotokana na shughuli za mafuta na gesi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.Kamati inaishauri Serikali kuliangalia upya suala hili na kufanya marekebisho yatakayoruhusu alau asilimia Fulani ya mapato hayo kubakia kwa maendeleo ya kampuni kwa nia ya kuifanya iwe kampuni imara zaidi na yenye kuaminika.
4. Kamati inaishauri Wizara kuratibu upatikanaji wa mafunzo maalum kwa watendaji wake wa ZPDC na ZPRA kutokana na ukweli kwamba taasisi hizi ni changa na zinahitaji kupata wataalamu wabobezi.

## 4.4 MAMLAKA YA KUDHIBITI UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA (ZANZIBAR PETROLEUM (UPSTREAM) REGULATORY AUTHORITY)

Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) imeanzishwa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia nambari 6 ya Mwaka 2016. Mamlaka hii imeanza kazi rasmi mwezi Machi 2017 kufuatia kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mamlaka. Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, shughuli kuu ya Mamlaka ni kusimamia na kudhibiti shughuli za Utafutaji, Uendelezaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

### CHANGAMOTO

1. Kutothibitishwa kwa muundo wa Mamlaka na Kamisheni ya Utumishi wa Umma jambo ambalo linaleta ukakasi kwenye utendaji wa shughuli za Mamalaka.Aidha, Maslahi ya watendaji wa Mamlaka hayaendani na uhalisia wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia duniani.
2. Uhaba wa wataalamu wabobezi kwenye fani ya Mafuta na Gesi Asilia.

3. Kukosekana kwa taarifa za Mafuta na Gesi Asilia zilizohifadhiwa TPDC (Legacy Data)
4. Ufinyu wa bajeti ya Mamlaka unaodumaza tafiti za kitaalamu.
5. Kukosekana kwa Eneo la kudumu la kutunzia Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR).
6. Mamlaka kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya mapato jambo ambalo linaikwaza Mamlaka kutokuwa na upeo wa mbali na maendeleo makubwa.
7. Maeneo yaliyoonesha matokeo chanya ya tafiti za awali za mafuta na gesi asilia (Kama na Tundauwa) kutoendelezwa na kuanza kuvamiwa na wananchi kwa ajili ya makaazi jambo ambalo linaweza kuigharimu Serikali wakati wa kuzichimba rasilimali hizo.
8. Uchakavu wa barabara inayotumika hadi kufika eneo la kisima cha awali cha Tundauwa.
9. Kamati imebaini kuwa hadi sasa wataalamu hawajaweza kugundua wapi haswa yalipo mafuta, walichoweza kugundua ni ishara tu za uwepo wa mafuta.
10. Zoezi la utafutaji wa mafuta na gesi kuchukua muda mrefu mno.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Mamlaka ijikite katika kutoa mafunzo kwa watendaji wake ili kuleta ufanisi kazini. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kutenga fungu maalumu kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ya mafuta na gesi ambapo asilimia Fulani ya fedha hizo itumike kwa ajili ya kuwajengea uwezo wataalamu wetu ili waweze kusimamia vyema rasilimali hizo kwa maslahi ya Taifa letu.
2. Kwa maslahi mapana ya Taifa letu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kuipa uzito Mamlaka hii na kuhakikisha suala la ucheleweshaji wa uingizwaji wa fedha ndani ya Mamlaka hii linaondoka kabisa.
3. Ingawa Mamlaka ina watendaji wazalendo walio tayari kuijenga nchi yao, Kamati inashauri Wizara kuyaangalia upya maslahi ya wafanyakazi wa Mamlaka hii

kutokana na ukweli kwamba kazi ya utafiti na uchimbaji wa mafuta huwaweka wataalamu muda mwingi kwenye mazingira hatarishi.

4. Kamati inashauri elimu itolewe kwa wanajamii wa Tundauwa na Kama juu ya taratibu za uchimbaji wa mafuta ili kuwatuliza wanajamii hao kutokana na shauku ya rasilimali ya mafuta na gesi asilia walionayo. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuyalinda maeneo hayo dhidi ya uvamizi wa wananchi kwa ajili ya makaazi jambo ambalo linahatarisha usalama wao.
5. Kamati inaiomba Serikali kuendelea na hatua ya Utafiti wa 3D ili hatimaye hatua nyengine zifuatiye na kufikia uchimbaji wa kisima cha majaribio ili kujua mustakbal wa nchi yetu kwenye rasilimali hizi muhimu.
6. Kamati inashauri Serikali kwenye kandarasi za uchimbwaji wa Gesi basi kampuni zitakazopaswa kupewa kandarasi hizo ni zile zinazojishughulisha na uchimbaji wa gesi na kuwa na uzoefu wa kazi hizo.

## 4.5 KAMPUNI YA MAENDELEO YA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA (ZANZIBAR PETROLEUM DEVELOPMENT COMPANY)

Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar imeanzishwa chini ya kifungu cha 32 cha Sheria Nambari 6 ya Mwaka 2016 ya Mafuta na Gesi Asillia na kusajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni Sheria Nambari 15 ya Mwaka 2013. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kampuni hiyo na kupokea taarifa ya utendaji wa shughuli zake.

### CHANGAMOTO

1. Uhaba wa wafanyakazi ni suala linaloikwaza kampuni kutokana na ukweli kuwa maendeleo ya sekta ya mafuta na gesi asilia yanahitaji kampuni ya Serikali iliyoimara kwenye Nyanja zote zikiwemo wataalamu wabobezi, miundombinu ya uhakika ili kuleta tija kwa Taifa.
2. Ufinyu wa Ofisi unaopelekea kutokua na mazingira mazuri ya kazi.
3. Kukosekana kwa wataalamu wabobezi katika sekta ya Mafuta na Gesi Asilia
4. Uelewa mdogo wa jamii juu ya sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Serikali kuratibu uajiri wa wafanyakazi wa Kampuni hii ili kuleta ufanisi kazini.
2. Kwa mnasaba wa majukumu mazito iliyokabidhiwa Kampuni, Kamati inaitaka Wizara kuiangalia upya Ofisi ya Kampuni hii na ikiwezekana iitafutie Kampuni eneo ambalo litaendana na hadhi yake.
3. Wizara, kupitia Kampuni ua Maendeleo ya Mafuta na gesi asilia itowe mafunzo elekezi ya mara kwa mara kwa wafanyakazi wa Kampuni hii ili kuwajengea ujuzi na hatimae kubobea katika kazi zao.
4. Kamati yangu inashauri Wizara kuengeza juhudi za kutoa elimu kwa jamii ili kuengeza uelewa juu ya masuala mazima ya Mafuta na Gesi

## 4.6 TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI

Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini Zanzibar (TUUMBZ) ni Taasisi yenye jukumu la kupanga na kusimamia kazi zote za tafiti zinazohusiana na Uvuvi na mazao ya baharini pamoja na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wavuvi, wakulima wa mwani, wanafunzi na wadau wengine. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi imeanzishwa April 2019 chini ya hati ya Sheria *(Legal Notice)* namba 32 ya kifungu 53 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 na Kifungu 55 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Act No. 2 ya 2011 kwa madhumuni ya kuendeleza tafiti za Uvuvi na mazao ya baharini ili kuimarisha Sekta ya Uvuvi nchini.

## CHANGAMOTO

1. Muundo wa Taasisi hii umeandaliwa kwa muda mrefu uliopita na umeshindwa kupata Baraka za Tume ua Utumishi Serikalini.
2. Kuchelewa kuundwa Bodi ya Washauri wa Taasisi hiyo kumekwamisha baadhi ya maamuzi muhimu.

3. Kukosekana kwa watafiti wenye ujuzi na uzoefu wa kuandika na kutangaza tafiti katika majarida ya Kitaifa na kuweza kubuni miradi sambamba na kufatilia ufadhili katika mashirika ya Kimataifa.
4. Taasisi bado ipo katika hatua ya maandalizi *(Establishment Phase)*, hivyo imechelewa kukamilisha Sheria ya Taasisi, Mpango Mkakati na agenda ya tafiti.
5. Wafanyakazi wa Taasisi hii wengi wao ni wapya na wanahitaji kupewa mafunzo mbali mbali yanayohusiana na masuala ya tafiti.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Taasisi hii kujikita sana katika masuala mazima ya kufanya tafiti, na hivyo kuajiri watendaji weledi ili kuleta ufanisi katika kazi.
2. Ili kufikia malengo tuliyojiwekea, Kamati inaiomba Wizara kuikamilisha Sheria ya Taasisi hiyo ili sasa Sheria hiyo iweze kutumika kuiongoza Taasisi na wadau wake.
3. Kamati inaishauri Serikali kuikamilisha mapendekezo ya Maslahi ya wafanyakazi wa Taasisi hii ili sasa wafanyakazi wetu wafanye kazi kwa weledi na ufanisi
4. Kamati inaishauri Serikali kuidhinisha Muundo wa Taasisi pamoja na kuundwa kwa Bodi ya Washauri wa Taasisi.

## 4.7 IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI

Idara ya maendeleo ya Uvuvi ina majukumu ya kuendeleza Uvuvi wenye tija na endelevu kwa kuhifadhi mazingira ya bahari Pamoja na rasilimali zake. Idara pia inawahudumia wavuvi, wafugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini, wakulima wa mwani na wadau wengine tofauti wanaojishughulisha na mazao ya baharini.

## CHANGAMOTO

1. Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya kutekeleza kazi zilizopangwa.

2. Uhaba wa wataalamu katika uzalishaji wa vifaranga vya Samaki na mazao mengine ya baharini.
3. Uharibifu wa mazingira unaosababishwa na Uvuvi haramu.
4. Kutokua na taaluma ya uvuvi kwa wavuvi wadogo wadogo.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kuongeza doria za baharini ili kupunguza au kukomesha kabisa uvuvi haramu
2. Kamati yangu inaishauri Idara ya Uvuvi na Mazao ya Baharini kujikita katika kutoa mafunzo kwa wavuvi wadogo dogo ili kuwaongezea taaluma na ujuzi juu ya masuala ya Uvuvi

## 4.8 KAMPUNI YA UVUVI (ZAFICO)

Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) ni Kampuni ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya makampuni *(Companies Act No. 15/20/13)*ya mwaka 2017. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Kampuni ya ZAFICO ikiwa ni katika kutekeleza Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050, MKUZA III na Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025. Malengo makuu ya kuanzishwa kwa Kampuni hii ni pamoja na "Uvuvi endelevu wa kibiashara, kuimarisha miundombinu ya Uvuvi, kuanzisha viwanda, kuongeza ajira na pato la Taifa kwa kuzingatia malengo na mikakati ya muda mrefu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuimarisha Sekta ya Uvuvi nchini pamoja na kukuza Uchumi wa Buluu.

Kampuni ya Uvuvi inaongozwa na mpango wake wa biashara (Business Plan) wa Mwaka 2018-2022, imeundwa na wanahisa wanne ambao ni:-

i. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kwa hisa ya 45%
ii. Shirika la Biashara la Zanzibar (ZSTC) kwa hisa ya 27%
iii. Shirika la Bandari la Zanzibar (ZPC) kwa hisa ya 18%
iv. Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) kwa hisa ya 10%

ZAFICO imeweza kubuni fursa ya miradi mikubwa minne ya biashara ambayo Kampuni itaweza kuwekeza. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

i. Uvuvi wa Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing)*
ii. Kiwanda cha kusarifu minofu ya Samaki na vyumba vya baridi *(An Integrated Processing and Cold Storage Facility)*
iii. Kiwanda cha kusarifu Dagaa *(Anchovy Processing Unit)*
iv. Mradi wa ufugaji Samaki baharini *(Cage Fish Culture)*

## CHANGAMOTO

1. Gharama za mafuta katika kuendesha shughuli za uvuvi wa bahari kuu ni sawa na asilimia 55 za gharama zote za uvuvi wa bahari kuu. Wakati ikionekana kua Meli za kigeni huondolewa kodi za mafuta ili kuweza kukabiliana na uvuvi wa bahari kuu, SEHEWA 02 imekua ikihitaji lita 5,500 kwa safari ya wiki mbili sawa na Tsh. 11,418,000.
2. Uzoefu wa uvuvi wa Bahari kuu unaendelea kua changamoto kwa wavuvi wetu visiwani. Matatizo kadhaa yanaendelea kujitokeza katika safari za uvuvi ikiwemo kujizonga kwa mishipi, kuliwa kwa chambo bila ya Samaki kunasa, kukatwa kwa ndoana na kupotea kwa mitego.
3. Upatikanaji wa chambo muafaka ni miongoni mwa changamoto kubwa katika uvuvi huu. Aina mbili za Samaki zilitegemewa kutumika kama chambo ikiwemo vibua na ngisi. Upatikanaji wa Samaki hawa katika soko la Zanzibar una changamoto zifuatazo ;-
    - Samaki hawa wapo sokoni kwa ajili ya matumizi ya chakula kwa hiyo wanauzwa kwa bei ya juu ukilinganisha na samaki wanaouzwa katika masoko ya kimataifa kama chambo. Kwa mfano, kilo ya Ngisi katika soko la Zanzibar ina bei mara mbili ya wale wanaouzwa kutoka nje kama chambo.

- Samaki hawa wanavuliwa kwa kiwango kidogo kwa siku na hivyo inachukua muda mrefu kuweza kukusanya kiwango cha kutosha kinachotakiwa kwa safari ya uvuvi. Hii inaongeza thamani ya chambo kwasababu kuna haja ya kuwahifadhi katika vifaa vya baridi kwa angalau siku saba.

4. Hali ya hewa imekua ni yenye kubadilika mara kwa mara ikiwemo mvua na upepo mkali. Hali hii imesababisha boti kurudi kabla ya muda uliopangwa na kuharibu mipango ya uendeshaji wa shughuli za uvuvi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Kampuni kujikita katika kutoa mafunzo elekezi ya mara kwa mara kwa wafanyakazi wake hususani mabaharia ambao wanasafiri kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu ili kupata mbinu na maarifa ya ziada katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.
2. Ili kuiwezesha Kampuni kupunguza gharama za uvuvi na kuongeza faida, Kamati inaishauri Serikali kuzipunguzia kodi za mafuta Boti za Uvuvi za Kampuni.
3. Kamati inaishauri Kampuni kujenga mahusiano mazuri na Mamlaka za hali ya Hewa ili kupokea taarifa za hali ya hewa kabla na wakati wote wa safari za boti za uvuvi.
4. Kamati yangu inaitaka Kampuni kuongeza wigo na ubunifu wa kuongeza mapato kwani hali ya mapato ya Kampuni hii hairidhishi kwa sasa.

## 4.9 AFISI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI – PEMBA

Kamati ilitembelea Wizara ya Uchumi wa buluu na Uvuvi Pemba mwezi Agosti, 2021 na kupokea taarifa ya utekelezaji wake.

## CHANGAMOTO

1. Wafanyakazi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa upande wa Pemba wanafanyakazi katika mazingira magumu ambapo ndani ya ofisi moja kunapatikana vitengo Zaidi ya kimoja.
2. Afisi ina uhaba wa vitendea kazi jambo ambalo linapunguza ufanisi wa kazi.
3. Kuna mlundikano wa vyombo chakavu ndani ya eneo la Afisi bila ya kushughulikiwa kwa matengenezo au kufanyiwa taratibu za kuuzwa.
4. Ndani ya eneo la Afisi, kuna nyumba ndogo ambayo inatumika kama *Rest House*kwa ajili ya wageni mahususi, lakini usalama wa eneo hilo ni mdogo kwani lipo wazi na halina ukuta.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kulitatua suala la uhaba wa upatikanaji wa vifaranga vya mazao ya baharini ili kuwapa moyo wafugaji wa mazao ya baharini na kukukza uchumi wetu kwa ufugaji wenye tija.
2. Kamati inaishauri Serikali kuratibu upatikanaji wa wafanyakazi katika Idara hii ili kupunguza uhaba mkubwa wa watendaji unaozorotesha shughuli za Idara.
3. Kamati inaishauri Wizara kuipatia Idara vyombo vya usafiri ili kufika kiurahisi na kwa wakati maeneo mbali mbali ya kazi.
4. Ili kuongeza ufanisi na kuendana na kasi ya Uchumi wa Buluu, Kamati inashauri Wizara kuratibu upatikanaji wa mafunzo kwa wafanyakazi wa Idara hii.
5. Kamati imesikitishwa na kadhia ya kuwepo kwa boti mbili tu za doria, boti ambazo kwa muda mkubwa hua hazina mafuta. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuimarisha sekta ya doria kwa upande wa Pemba. Halkadhalika Kamati inaitaka Wizara kuweka fungu maalum la fedha kwa ajili ya mafuta ya doria ili kupambana na uvuvi haramu kwa ufanisi.

## 4.10 IDARA YA UVUVI – PEMBA

## CHANGAMOTO

1. Idara ya Uvuvi – Pemba ina wafanyakazi wachache sana kwa wilaya zote nne (4) za Pemba

| S/No | WILAYA | WALIOPO | MHITAJI | UPUNGUFU |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Micheweni | 2 | 13 | 11 |
| 2 | Wete | 3 | 8 | 5 |
| 3 | Chake chake | 3 | 10 | 7 |
| 4 | Mkoani | 3 | 13 | 10 |
| | **Jumla** | **11** | **44** | **33** |

2. Kwa muda mrefu wafanyakazi wa Idara hii hawajapatiwa mafunzo ya aina yoyote jambo linalopunguza ufanisi wa kazi.
3. Idara ina uhaba wa vyombo vya usafiri jambo linalopelekea kutofika kwa wakati katika maeneo mbali mbali ya Kazi.
4. Idara ina Boti mbili (2) tu za doria, idadi ambayo ni ndogo na haiendani na kasi ya dhana nzima ya Uchumi wa Buluu. Kadhalika, kumekua na utaratibu mbaya wa upatikanaji wa mafuta ya boti hizo kwa ajili ya shughuli mbali mbali ikiwemo kupiga doria.
5. Kitengo cha mazao ya baharini kina uhaba mkubwa wa vifaranga hali inayopelekea wafugaji wa mazao ya baharini kubaki muda mrefu bila ya kupata vifaranga.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kulitatua suala la uhaba wa upatikanaji wa vifaranga vya mazao ya baharini ili kuleta uwekezaji wenye tija.
2. Kamati inaishauri Serikali kuratibu upatikanaji wa wafanyakazi katika Idara hii ili kupunguza uhaba mkubwa wa watendaji.
3. Kamati inaishauri Wizara kuipatia Idara vyombo vya usafiri ili kufika kiurahisi na kwa wakati maeneo mbali mbali ya kazi.
4. Ili kuongeza ufanisi na kuendana na kasi ya Uchumi wa Buluu, Kamati inashauri Wizara kuratibu upatikanaji wa mafunzo kwa wafanyakazi wa Idara hii
5. Kamati imesikitishwa kwa kuwepo kwa boti mbili tu za doria, boti ambazo kwa muda mkubwa hua hazina mafuta na inashauri Serikali kuimarisha sekta ya doria kwa upande wa Pemba. Halkadhalika Kamati inaitaka Wizara kuweka fungu maalum la fedha kwa ajili ya mafuta ya doria ili kupambana na uvuvi haramu kwa weledi na ufanisi.

## 4.11 SOKO LA TUMBE

Ni soko la kisasa ambalo limejengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuwaondolea usumbufu wananchi wa Tumbe na vijiji jirani katika shughuli zao za uvuvi ambazo ndio tegemeo kuu la kuendeshea maisha yao. Kamati ilitembelea soko hilo na kupokea taarifa ya uendeshaji wake.

## CHANGAMOTO

1. Soko lina changamoto kubwa ya mfumo wa kupitisha hewa safi ambapo hakuna sehem kubwa ya kupitisha upepo na limejengwa kwa urefu wa kawaida.
2. Soko lina mtambo wa barafu lakini mpaka Kamati inalitembelea soko hilo, mtambo huo ulikua haujaanza kutumika licha ya kuwa tayari umeshafungwa na hauna hitilafu yoyote. Aidha, ikitokezea hitilafu yoyote kwenye mtambo huo, utengenezaji wake hautokua ndani ya wakati kutokana na kukosekana kwa fundi wa mtambo huo ndani ya Soko.

3. Masanduku ya kuhifadhia barafu hayapo ndani ya chumba maalum cha kuhifadhia masanduku hayo kutokana na masanduku hayo kutopita katika mlango wa chumba kilichotengwa kwa ajili ya kuhifadhi masanduku.
4. Kuna wavuvi wa meli kubwa huwa wanaenda katika visiwa vidogo karibu na Tumbe na kuchimba mchanga kwa ajili ya kufunga vipolo vya mchanga na nyavu zao ili nyavu zao za uvuvi ziende kima kirefu, hali ambayo inasababisha uharibifu wa mazingira.
5. Hakuna boti za uokozi katika eneo hilo hali inayopelekea kuchelewa kuokolewa wavuvi endapo wakipata hitilafu wakati wakiwa katika shughuli zao za uvuvi.
6. Wafanyabiashara wa dagaa wa Tumbe wana changamoto ya miundombinu ya kuhifadhia dagaa ambapo kipindi chamvua kubwa dagaa hilo huharibika na kupelekea wafanyabiashara hao kuingia kwenye hasara kubwa.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kuandaa mkakati maalum wa kuwaelimisha wananchi juu ya manufaa ya kulitumia soko hilo na kuhamasisha ulipaji wa tozo zitakazotokana na soko hilo kwa manufaa ya jamii na Serikali
2. Upatikanaji wa boti ya uvuvi kwa wavuvi wa Tumbe ni jambo la msingi sana. Hivyo Kamati inashauri Wizara iwapatiye boti hiyo wavuvi wa Tumbe ili iweze kuwasaidia wakati wa dharura.
3. Wizara inapaswakutafuta njia ambazo litaifanya soko la Tumbe kupitisha hewa vizuri.
4. Kamati inaishauri Wizara kumuajiri mtaalamu wa mtambo wa barafu ili kuwa na uhakika wa barafu sokoni hapo.
5. Kutokana na mazingira magumu ya waanika dagaa, Kamati inaishauri Wizara kuwapatia nyenzo za kukaushia dagaa kitaalamu pamoja na kuwapatia miundombinu ya kuhifadhia dagaa.

## 4.13 UKULIMA WA MWANI

Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi ilikutana na kikundi cha wema hauozi kilichopo Makangale kilichoanzishwa mwaka 2004 kwa kuanza kulima mwani kwenye maji madogo lakini baada kulima kwa muda mrefu bila ya mafanikio mnamo mwaka 2021, Serikali Ya Mapinduzi Zanzibar kupitia taasisi yake ya utafiti na uvuvi na mazao ya baharini iliwapatia mafunzo wakulima hao kulima kilimo cha mwani kwenye kina kirefu,hali ambayo imewapelekea wakulima kupata mavuno mengi ukilinganisha na awali. Hali hiyo imepelekea wananchi wengi wa eneo hilo kuhamasika kwenye kulima kilimo cha mwani na idadi ya wananchi waliojiunga kwenye kikundi hicho kuongezeka na kufikia idadi ya watu 28 hadi sasa.

## CHANGAMOTO

1. Kamati imegundua kwamba kikundi hicho na jamii iliozunguka eneo hilo hawana kabisa elimu inayohusiana na mikopo.
2. Kamati Imebaini wanakikundi cha Wema Hauozi na Jamii iliolizunguka eneo hilo wanatamani kujiunga na mifuko ya hifadhi za jamii hasusan ZSSF ili wapate manufaa baadae lakini pia hawana uelewa na jinsi ya kujiunga na mifuko hiyo.
3. Kamati imebaini kuwepo kwa mgogoro wa njia baina ya wananchi wa eneo hilo la Makangale na Mwekezaji mzalendo wa Hotel ya Pemba Paradiseambae amewazuwia wananchi kutumia njia iliyopita pembezoni mwa hoteli yake na kuwalazimisha kuzunguka kwenye njia isiyopitika na kupelekea wamanchi kujihisi wanyonge kwenye ardhi yao.
4. Kumekuwa na changamoto ya barabara katika eneo hiloinayowasababishia wakulima kupata taabu kwenye kusafirisha mavuno ya mazao ya baharini.
5. Kamati imebaini kuwepo kwa boti moja tu aina ya fiber, hali ambayo husababisha zoezi la kupanda mwani na kuushughulikia kuchukua muda mrefu.
6. Kamati imegundua kukosekana kwa soko la uhakika la kuuzia mwani katika kisiwa cha Pemba.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Mara baada ya kutembelea eneo la ujenzi wa kiwanda cha mwani, Kamati imesikitishwa sana na eneo hilo kutokuwa na maendeleo yoyote ingawa kuna maagizo ya Serikali kwa taasisi nne kuchangia ujenzi wa kiwanda hicho. Hivyo, Kamati inaiomba Serikali kumaliza mipango yake ya ujenzi wa kiwanda hicho ili hatimaye ujenzi ufanyike.
2. Wizara inayohusika na mambo ya Ardhi na maakazi, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Wizara inayohusika na utalii kwenda kwenye eneo la makangale ambapo kuna mgogoro wa njia baina ya muekezaji wa hoteli ya Pemba Paradise na wananchi wa eneo hilo.
3. Kutokana na kiu ya wakulima wa mwani kupata maendeleo ya haraka kupitia sekta hii, Kamati inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuharakisha zoezi la ununuzi na ugawagaji wa boti 500 za uvuvi.
4. Kamati inaiagiza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kutoa elimu kwa wanakikundi cha wema hauozi na jamii yote ya eneo hilo, inayohusiana na mikopo pamoja na namna yakuchangia kwa hiyari kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii (ZSSF).

## 4.14 MAMLAKA YA UVUVI WA BAHARI KUU

Ni taasisi ya Muungano ambayo inasimamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mapato ya Mamlaka hii yanagawiwa kwa asilimia 40 kwa 60 kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

## CHANGAMOTO

1. Ingawa tatizo sugu la kutokuwa na uhalali sheria ya Uvuvi wa Bahari Kuu kutumika Zanzibar limetatuka bado Mamlaka inakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na Sera ya Uvuvi wa Bahari kuu.

2. Mamlaka haina watumishi wa kutosha ambapo baadhi ya watumishi waliopo wameombwa katika Ofisi za Srikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT).
3. Kamati imejionea uchakavu wa jengo la mamlaka ambapo baadhi ya sehemu zinavuja, kuna sehemu nyengine "*Tiles*" zimetoka na kukosekana kwa umeme kwa baadhi ya sehemu za jengo
4. Mamlaka haina boti za doria ambazo ni kitendea kazi muhimu kwa mujibu wa shughuli zake za kila siku.
5. Mamlaka haina tafiti za kutosha zinazohusuana na masuala mazima ya bahari kuu.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati imesikitishwa kuarifiwa kua Taasisi hii ina wafanyakazi 32 tu ambapo wafanyakazi hao wote sio wa Mamlaka bali ni waajiriwa wa SMT na SMZ na wameazimwa tu ndani ya taasisi hiyo. Hivyo, inaitaka Mamlaka kuanza taratibu za kuajiri watendaji.

2. Kamati inapendekeza kufanyika kwa tafiti za kutosha kwenye uvuvi wa bahari kuu kwa ajili ya kuimiarisha Taasisi hii.

3. Kamati imejionea uchakavu mkubwa wa jengo la Mamlaka, hivyo kunahitajika ukarabati mkubwa ili jingo hilo lirudi katika hadhi yake.

## 4.15 MRADI WA SWIOFISH

Mradi wa Usimamizi wa Shughuli za Uvuvi wa Kanda ya Kusini Magharibi ya Bahari ya Hindi (SWIOFish) ni Mradi wa miaka sita uanofadhiliwa na Benki ya Dunia. Mradi huu ulianza rasmi tarehe 22 Juni, 2015 na ulitarajiwa kumalizika tarehe 30 Septemba, 2021 lakini umeongezewa muda hadi Septemba, 2022. Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuinua hali za kiuchumi, kijamii, na kimazingira kwa jamii zinazoishi katika ukanda wa kusini magharibi mwa bahari ya hindi (SWIO Countries) kutokana na uvuvi endelevu (uliopewa kipaumbele (sustainable marine fisheries). Mradi huu nchini Tanzania

unatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Tanzania Bara chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania pamoja na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Zanzibar chini ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.
Kati ya Miradi ya SwioFish ambayo Kamati imeikagua ni pamoja na Soko la Nungwi, Jengo la ZAFIRI na Soko la Tumbe.

## CHANGAMOTO

1. Kamati imearifiwa kukamilika kwa mfumo wa ukusanyaji taarifa za uvuvi ambao unajulikana kama SAMAKIS na unapatikana kupitia wavuti http://167.71.187.181/samakis.php, lakini wavuti hiyo haifanyi kazi na kuibua maswali mengi juu ya ufanisi wa upokeaji na uhifadhi wa taarifa za uvuvi.

2. Kamati imearifiwa kua soko la Nungwi lilitengewa jumla ya shilingi 260,000,000 milioni kwa ajili ya ujenzi mpya lakini wananchi wa eneo hilo wamelalamika kua soko limefanyiwa ukarabati tu badala ya kujengwa upya.

3. Soko la Nungwi halina chumba cha baridi na mashine ya kutengezea barafu kwa ajili ya shughuli za Soko.

4. Kamati imearifiwa kuwa wakati wote wa ujenzi Wizara haikuwashirikisha wananchi wa kijiji cha Nungwi ambao ndio watumizi wakuu wa soko hilo.

5. Soko halina boti za dharura wala doria na endapo ikitokea hitilafu yoyote wakati wavuvi wakiwa katika shughuli zao za uvuvi hawawezi kupatiwa msaada wa haraka.

6. Kamati imearifiwa kua kazi kuu ya taasisi hii ni kufanya tafiti, lakini mpaka sasa kuna uhaba mkubwa wa watafiti na kupelekea shughuli hiyo muhimu kutofanyika.

7. Kamati imearifiwa kua vifaa vya maabara vinavyotakiwa ndani ya jengo la ZAFIRI ni nusu tu ambavyo vitanunuliwa na mradi wa SwioFish na vilivobakia Wizara itaratibu upatikanaji wake.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa ajili ya utendaji bora wa soko la Nungwi, Kamati inaiomba Wizara kuratibu upatikanaji wa machine za kutengezea barafu, lakini pia kupatikana kwa chumba cha baridi kwa ajili ya kuhifadhia samaki.

2. Kamati inaishauri Wizara kuratibu upatikanaji wa boti za dharura ili kuhakikisha usalama wa wavuvi wakiwa katika shughuli zao za kila siku.

3. Kamati imesikitishwa na kitendo cha kutoshirikishwa wananchi wa Nungwi kwenye mipango ya matengenezo ya soko la Nungwi. Kimsingi wananchi hao ndio watumizi wa soko hilo na suala la kutowashirikisha linaweza kuleta migogoro isiyo ya lazima baina ya Serikali na wananchi wake. Hivyo, Kamati inaitaka Wizara kurekebisha kasoro hii na kuhakikisha jambo kama hili halitokei tena kwenye miradi mengine.

4. Kamati inapongeza kwa juhudi za kuliwezesha Jengo la ZAFIRI kuwa na vyanzo vitatu vya umeme ambavyo ni umeme wa ZECO, Generator pamoja na Solar. Hata hivyo, ni wajibu wa Wizara kuratibu upatikanaji wa vifaa vilivobakia vya maabara ili kuleta ufanisi kwenye kazi za tafiti za ZAFIRI.

5. Kamati inaishauri taasisi kutoa miongozo ya aina ya uvuvi na utaratibu kwa wavuvi ambao wanataka kuvua katika maeneo ya hifadhi ili kuwapa fursa wananchi kufanya shughuli zao bila ya kuharibu mazingira.

6. Taasisi ya ZAFIRI ina uhaba wa wataalamu wa kufanya tafiti, Kamati inaishauri Wizara kuratibu upatikanaji wa wataalamu ambao watasaidia kufanya tafiti kwa mafanikio makubwa. Aidha, Kamati inasisitiza suala zima la kuzihifadhi taarifa zetu za utafiti katika sehemu salama.

## 4.16 SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA (TPDC)

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limeanzishwa mnamo mwaka 1969 na kuanza shughli zake rasmi mnamo mwaka 1973. Kamati imelitembelea Shirika hilo kwa

madhumuni ya kujifunza lakini pia kuimarisha mahusiano na ushirikiano kati ya TPDC na Taasisi zetu zinazohusiana na masuala mazima ya Mafuta na Gesi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kupitia TPDC, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefaidika katika kugundua na kuendeleza masuala ya mafuta na gesi pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam wa maendeleo ya mafuta na gesi. Kamati inashauri Serikali kuiwezesha ZPDC kufanya kazi zake kitaalamu na kuisaidia Serikali katika masuala mazima ya Mafuta na Gesi.

2. Katika kuvifanyia utafiti vitalu vya baharini, kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa fedha za kutosha na teknolojia ya kisasa. Kwa mnasaba huo, kunahitajika uwekezaji mkubwa sana katika vitalu vya baharini hali ambayo itapelekea kufikia malengo yetu endapo ZPDC haitowezeshwa kikamilifu

3. Kuna makubaliano (MOU) ambayo yanaonesha eneo la ushirikiano na kwa mara kadhaa TPDC hua inawaalika ZPDC katika mafunzo pamoja na field work ya kusoma data. Lakini kuna changamoto kubwa ya uhaba wa fedha kwa upande wa ZPDC. Hivyo Kamati inaisisitiza Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kufanya juhudi za makusudi ili wataalamu wetu wa ZPDC waweze kushiriki kwenye mafunzo hayo muhimu.